Nipashe
Jumatatu Oktoba 14, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580048
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper




UKURASA 13



## Chadema yafunguka Lissu kurejea nchini

UKURASA 2

# FAO yatahadharisha Tanzania ulaji ovyo

**YAELEZA** jinsi wengi walivyo hatarini kukumbwa magonjwa yasiyoambukiza ...*Endelea ukurasa wa 2*



Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Uwekezaji), Dorothy Mwaluko, akimsikiliza mmoja wa askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Konstebo Mary Messo, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Upunguzaji wa Athari za Maafa Duniani jijini Dodoma jana. **PICHA: ZIMAMOTO NA UOKOAJI**

## Muda wa kujiandikisha uchaguzi mitaa waongezwa

UKURASA 3


## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**VIBALI VYA UAGIZAJI MBOLEA NJE KUFUTWA**
SERIKALI imesema baada ya miaka mitatu ijayo inatarajia kufuta vibali vyote vya kampuni zinazo...

UKURASA WA 4

**JULIUS NYERERE: SHUJAA ALIYEKAMATA BARA AFRIKA**
MWALIMU Julius Nyerere alizaliwa kijijini Butiama, Aprili 13, 1922 na alifariki Oktoba 14, 1999 katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas mjini London...



UKURASA WA 8

**SERIKALI YAKATAZA KUFUKUZA WANAFUNZI KARIBIA MITIHANI**
SERIKALI imepiga marufuku tabia ya baadhi ya shule...


## Mafuriko yaua 5, mamia wakosa makazi

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA KUITAFUTIA PUMZI PYRAMIDS KWA PAN AFRICANS UK. 31

**MAONI, KATUNI UK.6**

## Mafuriko yaua watoto watano

**Na Dege Masoli,** KOROGWE

WATOTO watano wamekufa maji kutokana na mafuriko wilayani Korogwe mkoani Tanga na kufikisha idadi ya waliofariki kufikia 12 mkoani hapa kutokana na mvua.

Aidha, kaya zaidi ya 300 zimekosa makazi kutokana na mvua hizo zinazoendelea kunyesha kwa takribani wiki mbili sasa katika maeneo mbalimbali ya mkoani Tanga.

Pia daraja la Mto Mandera lililopo Kata ya Segera mpakani mwa Wilaya za Handeni na Korogwe mkoani Tanga limekata mawasiliano ya barabara kati ya mitano ya Tanga, Dar e Salaam, Arusha, Pwani na Manyara na kusababisha magari zaidi ya 200 kukwama kwa zaidi ya saa 36, huku abiria takribani 800 wakilala nje.

Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Kissa Gwakisa, alisema mafuriko hayo yametokea katika Kitongoji cha Magunga - Mzia Kata ya Foroforo baada ya nyumba iliyokuwa na watu wanane wa familia moja nyumba yao kuanguka na watoto watano kati yao kusombwa na maji ambapo kati yao miili yote mitano imepatikana.

Kufuatia hali hiyo, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Korogwe ilifika katika kijiji hicho pamoja na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambapo kwa kushirikiana na wananchi wamefanikiwa kufukua miili ya watoto hao iliyofunikwa na mchanga usiku wa kuamkia jana.

Gwakisa alisema watu 120 ambao makazi yao yamezingirwa na maji wamehifadhiwa katika kambi maalum kijijini hapo, na ametoa tamko la watu kutokurudi katika makazi yao hadi tamko la serikali hata kama hali itarejea kuwa ya kawaida.

Barabara zilizoathirika ni ya Kwashemshi-Dindila-Bungu kutokea Jimbo la Bumbuli wilayani Lushoto, ambapo kulianguka mawe makubwa yaliyoziba njia katika bonde la Kwang'andu ambapo mbunge huyo alifika hapo Ijumaa kuanzia majira ya asubuhi hadi mchana kusimamia shughuli ya kuondoa mawe na tingatinga.

Barabara nyingine zilizoharibika ni za Lewa -Lutindi, Makuyuni-Bungu, Dindila -Mpale na Mswaha. Eneo jingine lililoharibika ni daraja la Kwashemshi -Dindila eneo la Kwakibili limesombwa na maji.

Mvua hiyo imeanza kuleta madhara katika kijiji cha Dindira kilichopo wilayani Korogwe ambapo watu saba walikufa kwa kusombwa na maji na kuziacha bila makazi zaidi ya kaya 300.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, Kwame Daftari, alisema kutokana na hali hiyo, magari yaliyokuwa yanasafiri kati ya Arusha na Dar es Salaam yanatakiwa yapitie njia ya Handeni kupitia Mkata wakati magari yanayofanya safari zake kati ya Tanga -Arusha, Tanga - Korogwe, Tanga - Lushoto yalisimama safari.

# Tanzania yapewa angalizo ulaji ovyo

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SHIRIKA la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), limetahadharisha Tanzania kuwapo ongezeko la idadi ya watu walio katika hatari ya kupata magonjwa sugu kutokana na mchanganyiko wa milo mibovu na maisha ya kutofanya mazoezi.

Magonjwa yaliyotajwa ni shinikizo la damu, kisukari, magonjwa ya moyo, kiharusi na aina fulani ya saratani kutokana na mchanganyiko wa milo mibovu na aina ya maisha ya kutofanyisha miili kazi na uzito uliopindukia pamoja na unene uliopitiliza.

Tahadhari hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mkazi wa FAO nchini, Fred Kafeero, wakati akiwasilisha hotuba yake katika ufunguzi wa mdahalo wa Siku ya Chakula Duniani kwa mwaka 2019 uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) mjini Morogoro.

Alisema walaji hususani wa mijini hawana muda wa kutosha kuandaa vyakula nyumbani, hivyo wamejikuta wakiingia katika maisha ya kisasa ambayo kwa kiasi kikubwa yanategemea ununuzi wa bidhaa katika maduka makubwa, sehemu za kuandaa vyakula kwa haraka barabarani na kwenye migahawa ambayo milo hiyo ina wanga mwingi, sukari, mafuta na chumvi ambavyo sio rafiki kwa afya.

Alisema kutokana na hali hiyo, wataalamu wa afya wametangaza kwa sauti ya juu kwamba milo mibovu ni sababu kuu ya vifo vitokanavyo na magonjwa yasiyoambukizwa yakijumuishwa magonjwa ya moyo, kisukari na aina fulani za saratani.

Akizungumzua kuhusu lishe duni, alisema kama ilivyo katika nchi kadhaa, Tanzania nayo ina tatizo la watu kuwa na lishe duni inayosababishwa na milo ya watu kupungukiwa na viini lishe muhimu ambavyo vinahitajika na mwili kwa ajili ya afya njema.

Kafeero alisema hali hiyo ya lishe duni imekuwa ikisababishwa na ugonjwa, malezi na lishe mbovu ya utotoni, uchafu wa mazingira pamoja na kutofikia huduma mbalimbali za kijamii ikiwamo majisafi.

Hata hivyo alisema moja ya majukumu ya FAO ni kutomeza utapiamlo katika hali zote na pia ndio muhimili wa lengo la maendeleo endelevu namba mbili ya dunia bila njaa, na kwamba itahakikisha inasaidiana na Serikali ya Tanzania kusaidia usalama wa chakula na lishe.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alisema bado kuna tatizo la uzito na unene uliopitiliza ukiongozwa na wanawake wenye viriba tumbo na kupanda kutoka asilimia 29.7 hadi kufikia 31.7 ambao wapo katika hatari ya kupata magonjwa hayo yasiyoambukizwa.

Akifungua mdahalo huo, Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, alisema licha ya Tanzania kujitosheleza na chakula kwa asilimia 120, lakini bado tatizo la lishe duni na udumavu bado ni changamoto kutokana na aina ya uzalishaji wa chakula katika maeneo husika.

Mwakilishi wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Neema Shosho, alisema wadau wa maendeleo wanaipongeza serikali kwa jitihada zake za kutokomeza tatizo la utapiamlo na udumavu kwa watoto na kutaka kuongezwa kwa elimu juu ya namna ya mfumo wa maisha kwenye matumizi ya chakula.



Mmoja wa wananchi wa Mkoa wa Morogoro akipata huduma ya kupimwa macho katika Hospitali ya Rufani ya mkoa huo, iliyotolewa bure na Klabu ya Lions kwa ufadhili wa kampuni ya M-bet. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Chadema yafunguka Lissu kurejea nchini

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimefunguka kuhusu usalama wa Mwanasheria Mkuu wake, Tundu Lissu, atakaporejea nchini kwa kueleza kuwa ni wajibu wa serikali kulinda raia wake.

Kutokana na hali hiyo, Chadema imeitaka serikali kutimiza wajibu huo kwa kuhakikisha Lissu anakuwa salama.

Akiongea na chombo kimojawapo cha habari nchini, Mkurugenzi wa Mambo ya Nje, Itikadi na Uenezi ya chama hicho, John Mrema, amesema wanaunga mkono uamuzi wa Lissu wa kutorejea nchini mpaka kwanza ahakikishiwe usalama wake.

"Kama chama, tunaunga mkono kauli yake kwamba kwa sasa tunataka athibitishiwe usalama wake pindi atakaporudi, na wenye mamlaka ya kuhakikisha usalama wake ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu ni wajibu wa serikali kulinda usalama wa raia wa mali zao," alisema.

Akizungumza katika chombo kimojawapo cha habari cha kimataifa wiki iliyopita, na kuulizwa kuhusu mpango wake wa kurejea, Lissu alidai kuwepo kwa maneno katika mitandao ya kijamii yenye vitisho, hivyo kutishia usalama wake endapo atarejea nchini.

"Wale walionipiga risasi 16 mchana wa saa saba katikati ya nyumba za serikali mjini Dodoma wakati wa kikao cha bunge bado wanaitwa watu wasiojulikana," alisema Lissu.

Akizungumzia kuhusu maneno yanayojitokeza katika mitandao ya kijamii yenye viashiria vya vitisho kwa usalama wake, Lissu alidai kuwapo kwa vitisho vya wazi vya baadhi ya watu kuwa atakaporudi nchini watu hao watamshughulikia.

"Kuna maneno yanajitokeza tokeza kwenye hii mitandao ya kijamii kwamba ngoja aje mara hii hatutakosea shabaha... kuna aliyetangaza kwenye televisheni mtandaoni kwamba Lissu akija atapigwa risasi," Lissu aliongeza.

Kuhusu hali yake ya kiafya Lissu alieleza

INAENDELEA UK. 8

HABARI KITAIFA

# Muda wa kujiandikisha S/Mitaa sasa waongezwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI leo ilikuwa ndiyo siku ya mwisho ya uandikishaji wa wapigakura kwenye daftari la orodha ya wapigakura, serikali imeongeza siku tatu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jafo, kazi ya uandikishaji wapigakura kwenye daftari la orodha ya wapigakura itamalizika Alhamisi, Oktoba 17, mwaka huu. "Waziri Jafo alitangaza kuongeza siku tatu za uandikishaji wa wapigakura kwenye daftari la orodha ya wapiga kura. Sasa zoezi hilo litakamilika Oktoba 17, mwaka huu," ilieleza taarifa hiyo.

**MILIONI 11 WAJIANDIKISHA**

Jafo alisema zoezi la uandikishaji limeendelea kupata mafanikio makubwa kwani hadi juzi zaidi ya watu watu milioni 11 waliweza kujiandikisha.

Jafo alisema wakati wa uandikishaji kulijitokeza changamoto mbalimbali kama vile kunyesha kwa mvua hali iliyosababisha watu kushindwa kujitokeza. "Kutokana na changamoto hiyo, kutokana na misingi ya utoaji wa haki na kwa kuzingatia masharti ya kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa, natoa mwongozo kuwa zoezi la uandikishaji linaongezwa siku tatu zaidi," alisema Jafo.

Wakati huo huo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda jana alitoa taarifa ikieleza kuwa kuanzia leo atatembelea katika baa na sehemu za starehe kufanya ukaguzi wa kuwabaini watu ambao hawajajiandikisha.

"Ndugu zangu wenye klabu, baa na sehemu zote za starehe naomba wahamasisheni watu wenu kwenye maeneo yenu kuhakikisha wamejiandikisha na kesho (leo) miongoni mwa maeneo nitakayoyatembelea ni pamoja na baa... ni matumaini yangu nikifika nitakukuta ukiwa tayari umejiandikisha," alisema Makonda.

Kazi ya uandikishaji wa wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu ilianza wiki iliyopita katika mikoa yote, lakini lilionekana kusuasua baada ya kuwapo kwa mwitikio mdogo wa wananchi kujitokeza.

Mkoani Dodoma, Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Binilith Mahenge, baada ya kujiandikisha kwenye kituo cha Nyerere, aliwaeleza waandishi wa habari kuwa matokeo ya uandikishaji katika Wilaya ya Kondoa ni 37,762.

Alieleza kuwa tangu kuanza kwa kazi ya uandikishaji ni wastani wa watu 2,000 tu kwa siku. Kadhalika, katika Jiji la Dar es Salaam, hususani katika maeneo ya Magomeni, Kimara, Ilala, Kiondoni wananchi walionekana kusuasua kujitokeza katika uandikishaji.

Mkoani Morogoro, hadi kufikia Oktoba 10, idadi ya watu waliojitokeza kujiandikisha ilikuwa ni 203,553 kati ya watu waliotarajiwa kuandikishwa1,423,111. Mikoa ya Dar es Salaam na Arusha ni miongoni mwa mikoa ambayo imeelezwa kuwa mwitikio wa wananchi kujiandikisha umekuwa wa kusuasua.

TANGAZO UK 26

# Vibali vya uagizaji mbolea nje kufutwa

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

SERIKALI imesema baada ya miaka mitatu ijayo inatarajia kufuta vibali vyote vya kampuni zinazoagiza na kuleta mbolea nchini.

Badala yake mbolea itakayokuwa inatumiwa na wakulima ni itakayozalishwa na viwanda vya nchini.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, aliyasema hayo jana, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani iliyofanyika kitaifa mkoani Katavi katika Manispaa ya Mpanda.

Alisema uamuzi huo utasaidia kufanya mbolea itakayokuwa inatengenezwa nchini kulingana na hali ya udongo uliopo tofauti na ilivyo sasa ambapo mbolea imekuwa ikiagizwa bila kujali aina ya udongo uliopo.

Alizitaka kampuni zenye vibali vya kuagiza mbolea nje zianzishe viwanda vya kuzalisha mbolea nchini.

Waziri Hasunga aliwasisitiza wadau wa maendeleo kuwaelimisha wakulima juu ya matumizi sahihi ya mbolea.

Aliiagiza mamlaka ya kuthibiti ubora wa mbolea kuhakikisha inakagua ubora wa mbolea yote inayoingizwa nchini kuanzia inapokuwa imefika bandarini na inapokuwa mikoani. Alisema kuanzia sasa kampuni zote ambayo zinaagiza mbolea nje ya nchi zinatakiwa kuwa na ofisi zao kwenye kila makao makuu ya mkoa na sio kuwa Dar es Salaam pekee.

Alisema Wizara ya Kilimo imeweka utaratibu wa kuhakikisha mbolea inawafikia wakulima kwa wakati kwani asilimia 90 inayotumiwa na wakulima nchini inatoka nje.

Waziri Hasunga alisisitiza wakulima wote kujisajiri kwenye daftari la wakulima ili waweze kutambulika nchi nzima idadi yao na uwezo wao wa kuzalisha mazao.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, alisema mkoa wake kwa sasa unashika nafasi ya nne kwa uzalishaji wa mazao ya chakula, hivyo lengo kwa msimu huu ni kushika nafasi ya kwanza katika uzalishaji huo.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS - IKULU

MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII



Julius Kambarage Nyerere
(1922 - 1999)

KUMBUKUMBU YA MIAKA 20 YA KIFO CHA BABA WA TAIFA,

MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE

Mwenyekiti, Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF wanaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Dkt. John Pombe Magufuli**, na Watanzania wote katika kumbukumbu ya miaka **20** ya kifo cha Baba wa Taifa, **Mwalimu Julius Kambarage Nyerere**

*TASAF itaendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano katika kupambana na umaskini kama ishara ya kuenzi mchango wa Mwalimu Nyerere dhidi ya umaskini.*

***PAMOJA TUONDOE UMASKINI***

Mkurugenzi Mtendaji

**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF**

S.L.P. 2719 Dodoma, Tanzania

Simu: +255 26 2963866 Nukushi: +255 26 2963871

Tovuti: **www.tasaf.go.tz**

Barua pepe: **info@tasaf.go.tz**

215455402

# Shujaa aliyekamata Bara la Afrika

Na Dk. Dalaly Kafumu

MWALIMU Julius Nyerere alizaliwa kijijini Butiama, Aprili 13, 1922 na alifariki Oktoba 14, 1999 katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas mjini London, Uingereza. Leo anakumbukwa kutimiza miaka 20 tangu kifo chake.

Ni siku inayowasha upya moto wa harakati za kuliunganisha Bara la Afrika, wakati yeye na wapiganiaji wengine wa Umoja wa Afrika; akiwamo Dk. Kwame Nkrumah wa Ghana, Patrick Lumumba wa Congo, Abdul Nasser wa Misri, Jommo Kenyatta wa Kenya, Ben Bella wa Algeria, Ahmed Sekou Toure wa Guinea, Leopold Sengor wa Senegal, Nelson Mandela wa Afrika Kusini, na wengineo. Miongo saba iliyopita waliwasha moto wa harakati za kuliunganisha Bara la Afrika kuwa nchi moja.

Viongozi waliokuwa miamba wa Umoja wa Afrika; walifikiri, kuona mbele na kutenda kwa umoja kulikomboa bara hilo kutoka ukoloni na hatimaye kuunganisha walichodhamiria - Jamhuri ya Muungano wa Afrika.

Tukiwa katika hoja na safari ya maisha yajayo kwenye Nchi ya Ahadi (Jamhuri ya Muungano wa Afrika); uwapo wa roho ya Mwalimu Nyerere maishani mwetu kijamii, kiuchumi na kisiasa katika Tanzania na Afrika ya leo; bado ni nguzo ya mwanga wa kutumikia njia iendayo kwenye neema.

Uwapo wa roho ya Mwalimu Nyerere katika maisha ya leo, unashuhudiwa na kila kiongozi wa kisiasa nchini anapojitambulisha na kunasibisha kwa uongozi na vitendo vya Mwalimu, lengo ni kuhalalisha na kubariki uongozi wake kwamba ni wa kizalendo, ili kuwashawishi wananchi wamkubali.

Pia uamuzi wa kanisa kumweka kwenye mchakato wa kuwa Mtakatifu, ni uthibitisho yupo kiroho miongoni mwetu, ukuu wa uongozi wake unadhihirika hadi sasa.

Mwalimu amekuwa na sifa ya wema, huruma na unyenyekevu, aliyethamini haki kwa wote, aliyefanikiwa kuanzisha Taifa la Tanzania lenye amani, umoja na mshikamano, akiyaunganisha makabila zaidi ya 120 yakaishi kwa umoja na kuongea lugha moja - Kiswahili.

Tangu miaka ya 1950 hadi 1990, Mwalimu Nyerere alitoa maisha yake kupambana na ukoloni, unyonyaji, ubaguzi wa rangi, ukabila, ukandamizaji, uonevu na kukosekana haki.

Aliongoza mapambano ya ukombozi wa Afrika kutoka mikono ya nyonyaji, ukoloni halisi na mamboleo.

Leo anapoenziwa kuwa mfano wa kuigwa katika maisha ya sasa, tunajivunia kuandika historia ya kuwa Baba wa Umoja wa Afrika, kiongozi kitaifa, na mtumishi wa Mungu.

Maneno na matendo yake, yameachia azma ya kuupata ukombozi na umoja wa Afrika, kutoka kumbukumbu ya maandiko ya viongozi wengi, wasomi na wanasiasa wa Afrika.

**ALIVYOPIGANIA AFRIKA**

Hotuba aliyoitoa katika Mkutano wa Kwanza katika kuanzisha Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) Mei 25, 1963 mjini Addis Ababa, Ethiopia, alionyesha utayari wa kuzisaidia nchi za Kiafrika zilizokuwa chini ya ukoloni kupata uhuru na mwisho kuziunganisha kuwa Afrika moja.

Alitamka: "Tumekuja hapa kutafuta mbinu za kulikomboa bara lote la Afrika...ili kuanzia sasa nchi za Afrika ambazo ni huru ziwasaidie ndugu zetu Afrika ambao hawajapata uhuru, waweze kupata uhuru..."

Pia kwenye mkutano huo alisali na wengineo mkutanoni kumwomba Mungu asaidie kuleta Umoja wa Afrika.

**ALIPONG'ATUKA**

Kwenye hotuba ya kuwaaga Watanzania alipong'atuka urais, Novemba 4, 1985, Nyerere aliyeamini katika Umoja wa Afrika, aliwashukuru Watanzania kwa uvumilivu pindi alipotumia muda mwingi, nguvu na rasilimali za taifa kusaidia mapambano ya kuikomboa Afrika.

Hata baada ya kustaafu, aliendelea kuamini katika Umoja wa Afrika.

**ALVYONG'ARA NJE**

Machi 6, 1997 kwenye sherehe ya miaka 40 ya Uhuru wa Ghana, mjini Accra, Ghana, Mwalimu alihutubia kuwataka viongozi wa sasa Afrika kupigania Umoja wa Afrika kwa nguvu mpya. Alisema: "Sisi viongozi wa wakati wangu tulilikomboa kisiasa Bara la Afrika. Nanyi viongozi wa sasa na wananchi wa Afrika kwa ujumla wenu, bebeni Mwenge wa Uhuru wa Afrika, muutie mafuta ya hamu na jitihada zenu ili muubebe kuufikisha kwenye umoja..."

Oktoba 16, 1997 akiongea na Bunge la Afrika Kusini mjini Cape Town, Mwalimu Nyerere, aliwakumbusha Waafrika kwamba, walihitaji umoja na kufanya kazi pamoja ili kujikomboa na utumwa wa kiuchumi.

Alinena: "Ni lazima tuihamasishe Afrika kujitegemea, ndani ya nchi mojamoja, lakini katika umoja wa nchi zote za Afrika. Kila nchi lazima itegemee rasilimali za nchi hiyo na rasilimali watu katika nchi hiyo ili kujiletea maendeleo."

Mwalimu anatambuliwa kuwa mpigania Umoja wa Afrika, aliyefanya hivyo kwa moyo mkuu na weledi wa hali ya juu.

Jacob Zuma, alipokiwa Makamu wa Rais wa Afrika Kusini, katika salamu za rambirambi kwenye msiba wa Mwalimu Nyerere aliueleza wasifu wake kuwa:

"Alitufundisha Waafrika kuhusu amani, demokrasia, na umoja; Mwalimu ni mpiganaia uhuru ambaye ni mmoja wa waasisi wa OAU, aliweka msingi madhubuti kwa Bara la Afrika wa kuanza safari ndefu kuelekea Amani na Umoja."

Pia Shubi Ishemo wa Shule ya Trinity and All Saints College ya Chuo Kikuu cha Leeds, Uingereza, mwaka 2000 aliandika kwenye Jarida la 'Review of African Political Economy Journal' akisifu umadhubuti wa Mwalimu Nyerere katika kupigania Uhuru wa Bara la Afrika. Anasema:

"Nafasi ya Mwalimu Nyerere kwenye ukombozi wa Bara la Afrika kati ya mwaka 1955 hadi 1990 ni alama isiyoweza kubatilika."

David Chaha wa Idara ya Lugha, katika Chuo Kikuu cha Egerton nchini Kenya, anamkumbuka Mwalimu Nyerere kwa matamshi: "Afrika inahitaji kutunza ndoto na maono ya Mwalimu Nyerere, ikiwa ni tunu na matumaini ya mafanikio yajayo ya watu wa Bara la Afrika."

Mnamo Januari 27, 2016, Marehemu Robert Mugabe, aliyekuwa Rais wa Zimbabwe na mshirika mkubwa wa Nyerere katika harakati za kupigania uhuru Kusini mwa Afrika, alipozindua kitabu kilichomhusu Mwalimu kitwacho: 'Julius Nyerere: Asante Sana, Thank you very Much' alimkumbuka rafiki yake akitamka: "Nyerere alikuwa na kazi kubwa ya kuzibeba nchi zote zilizokuwa zinapigania uhuru."

Julius Malema, kiongozi wa siasa za upinzani nchini Afrika Kusini alipohutubia mnamo Mei 25, mwaka jana, alienzi nafasi ya Mwalimu Nyerere katika ukombozi wa Afrika Kusini dhidi ya ubaguzi wa rangi.

Katika kusherehekea kumbukumbu ya Siku ya Watakatifu Mashahidi wa Uganda, Jumapili ya Juni 3, mwaka jana katika eneo la Namgongo nchini Uganda, Rais wa Uganda Yoweri Museveni, mfuasi shupavu wa Mwalimu Nyerere, kwenye sala ya kuombea mchakato wa kumtangaza Mwalimu Julius Nyerere kuwa Mtakatifu, alimweleza kuwa: " Mkatoliki na mzalendo na baba wa kweli wa Umoja wa Afrika na kiongozi mkuu; kwa nini tusimwite mtakatifu, aliyefanya kazi ya kutuunganisha sote. Alituleta pamoja kama Waafrika na hilo linamfanya awe wa pekee..."

***Mwandishi wa makala hii Mbunge wa Igunga na Kamishna wa Madini mstaafu**



Mwalimu Nyerere kulia akiwa na Samora Machel. **PICHA: MTANDAO**


Enabel

**Enabel – SAKIRP - Vacancy**

**Gender and microfinance specialist - Kigoma region**

Enabel – the Belgian Development Agency is recruiting a gender and microfinance specialist for its Sustainable Agriculture Kigoma Regional Project.

| | |
|---|---|
| **Duty station:** | Kigoma region – based at Kasulu Town with occasional travel to other districts |
| **Contract term:** | 1 year extendable - competitive salary package. |
| **Profile:** | minimum of degree in business studies, microfinance, agricultural economics, sociology or related area |
| **Experience:** | minimum of one year hands-on in microfinance and promoting women economic inclusion. Computer literate and good reporting skills in English/ Kiswahili. |

**Details vacancy at:**
**https://btctanzania.wordpress.com/**

**Submit your applications to:**
**recruitment.tza@enabel.be**

**Deadline: all applications should be submitted by 31 October 2019.**

**Only shortlisted candidates will be contacted.**

215455202

## KUMBUKUMBU MIAKA 20 KIFO CHA NYERERE

# Nyerere alivyotafsiri vitabu Kiswahili

**Na Jovina Bujulu, MAELEZO**

IKIWA miaka 20 sasa tangu kifo cha mwasisi wa Taifa la Tanzania Mwalimu Julius Nyerere kitokee, tunayo mengi ya kumkumbuka, ikiwamo mapenzi yake kwa lugha ya Kiswahili. Hivyo, unapokitaja Kiswahili, huwezi kuacha kutaja nafasi yake katika kuikuza fasihi hii.

Mwalimu alituachia urithi mkubwa na muhimu mno wa lugha ya Kiswahili, kwa kuifanya lugha ya Taifa mnamo mwaka 1967 na lugha ya Afrika Mashariki nzima. Kutokana na mapenzi yake kwa lugha hii, Mwalimu alitamani siku moja ingekuja kuwa lugha inayotumiwa na Waafrika wote na baadaye ngazi ya duniani pote.

Jitihada za Mwalimu zilifanya lugha ya Kiswahili itumike katika kampeni za kudai uhuru, sera za TANU pia ziliandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

Lugha hii iliwaunganisha wananchi wote kupiga vita ukoloni kwa njia ya nyimbo, mashairi na ngonjera. Katika kuhakikisha lugha hii inazidi kupata mashiko, serikali iliruhusu kuanzishwa kwa asasi mbalimbali zilizoshughulikia ukuaji na ueneaji wa Kiswahili. Asasi hizo ni pamoja na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), Chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA) na Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA). Katika kuonyesha thamani ya lugha hii, serikali ilitoa tamko la kutumia Kiswahili kama lugha rasmi bungeni na kutangazwa kuwa lugha rasmi ya Taifa, mnamo mwaka 1962. Ni hatua iliyofuatiwa na uteuzi wa Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katika shule za msingi nchini mwaka 1965.

Katika medani ya fasihi, Mwalimu Nyerere anajulikana zaidi kwa kutafsiri vitabu vya William Shakespear vya 'The Merchant of Venice' kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili akaviita 'Mabepari wa Venisi' na 'Julius Caeser' kuwa 'Julius Kaizari.'

Mapenzi yake kwa lugha hii yanajipambanua zaidi baada ya kuruhusu tamthilia za vitabu hivyo kuchezwa kwenye redio Sauti ya Unguja kwa lugha ya Kiswahili, bila kuwatoza malipo yoyote.

Mchango wa tafsiri za Mwalimu Nyerere, katika maendeleo ya Kiswahili ni pamoja na kukuza fasihi ya Kiswahili. Hiyo imo katika kupanua kiwango cha fasihi yenyewe, kwa sababu maandishi hayo mara nyingi yanawakilisha matokeo ya urithi wa vizazi kwa vizazi.

Tafsiri hizo pia zimechangia kukuza msamiati ambao kwa kawaida tafsiri za kigeni, aghalabu huingiza katika lugha lengwa maneno ya kigeni yanayokopwa pamoja na dhana zake kutoka lugha chanzo. Mchango mwingine wa tafsiri, ni pamoja na kuwahamasisha na kuwatia moyo watafsiri wengine wazalendo wa Tanzania kutumia maandiko mengine ya kitaalamu kwa manufaa ya jamii yetu.

Mfano huu ni mwanasiasa Paul Sozigwa, aliyefanya kazi kwa karibu na Mwalimu Nyerere, alitafsiri kitabu cha fasihi cha 'Song of Lawino' na cha 'Sayansi ya Uchumi' (The North South Dialogue).

Pia Mwalimu Nyerere, alitumia tafsiri ya kishairi katika utenzi wa Injili katika kitabu kitakatifu cha Biblia.


Pamoja na kutafsiri vitabu hivyo, mwalimu aliandika vitabu mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili ambavyo vilikuwa vinahamasisha wananchi kujiletea maendeleo yao, elimu ya kujitegemea, siasa na uchumi. Vitabu hivyo ni pamoja na: Uhuru na Umoja; Uhuru na Ujamaa; Uhuru na Maendeleo; na Azimio la Arusha. Viingine ni Elimu ya Kujitegemea; Miaka 10 ya Uhuru; Makala za Ujamaa; na 'Ukombozi wa Afrika.

Kwa kutambua umuhimu wa lugha ya Kiswahili, kikao cha 39 cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kilichofanyika hivi karibuni nchini kimempa heshima kubwa Mwalimu Nyerere, aliyekifanya Kiswahili kuwa lugha ya ukombozi, ikiwa ni rasmi katika mawasiliano ya SADC, baada ya Kiingereza na Kireno.

Katika kikao hicho, Mwenyekiti Rais Dk. Magufuli alisema kwamba kwa sasa lugha ya Kiswahili ni ya 10 kuzungumzwa duniani, huku pia ikiwa na nafasi kubwa sana barani Afrika na ndani ya SADC.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA (TASAC)

KUMBUKUMBU YA MIAKA 20 YA KIFO CHA BABA WA TAIFA MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE, OKTOBA 14, 1999 – OKTOBA 14, 2019



*Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere*

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa **SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA (TASAC)** tunaungana na Watanzania pamoja na familia ya Baba wa Taifa kwa kuadhimisha miaka 20 ya kumbukumbu ya kifo cha Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kilichotokea tarehe 14/10/1999.

**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA (TASAC)** tutamkumbuka Baba wa Taifa kwa busara, hekima na alivyojenga misingi ya umoja wa kitaifa na kudumisha amani na mshikamano kwa Watanzania na Afrika kwa ujumla.

Tutakukumbuka Daima Baba wa Taifa la Tanzania na Mwanamapinduzi shupavu wa Afrika.

215458202

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga puuzeni kelele za chura mkijiandaa Caf

**HATIMAYE** wawakilishi wa Tanzania katika michuano ya kimataifa, Klabu ya Yanga imeanza maandalizi ya mechi yao ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kumfahamu mpinzani wao.

Yanga imeangukia Kombe la Shirikisho baada ya kutolewa na Zesco ya Zambia kwenye raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Na tayari Shirikisho la Soka Afrika (Caf), lenye dhamana na michuano hiyo, limeshaendesha droo ya michuano hiyo ambapo Yanga itakutana na Pyramids ya Misri ikianzia nyumbani katika Uwanja wa CCM Kirumba Oktoba 27, mwaka huu kabla ya kurudiana wiki mbili baadaye.

Na endapo Yanga itapata matokeo ya jumla katika mechi hizo mbili nyumbani na ugenini, itafuzu moja kwa moja hatua ya makundi.

Hata hivyo, baada ya droo hiyo kupangwa kumekuwapo na maneno mengi kutoka kwa wachambuzi wa soka wengi wakiamini, huo ndio mwisho wa safari ya Yanga kimataifa kwa msimu huu.

Vitisho, au kujiaminisha kwa wanaovitoa kwa Yanga ni kutokana na uimara wa kikosi cha Pyramids ambacho kinaundwa na wachezaji kutoka Brazil na Colombia.

Na si suala tu la kwamba wanatoka nchi hizo zilizopiga hatua kubwa kisoka, bali pia wanaamini wachezaji hao sita ambao gharama ya kuwanunua ni zaidi ya Sh. bilioni 80 za Tanzania, inamaanisha ni wa daraja la juu ukilinganisha na nyota wanaounda kikosi cha Yanga.

Pia kitendo cha Pyramids hadi sasa kushika nafasi ya pili nyuma ya vinara, Al Ahly kwenye msimamo wa Ligi Kuu Misri kunawafanya wengi waamini Yanga haitaweza kupenya hatua ya makundi.

Lakini pamoja na hayo yote, Nipashe tunaamini mpira hauchezwi kwa kuangalia gharama ya wachezaji husika kikosini wala nchi wanapotoka au nafasi yao kwenye ligi ya nyumbani.

Ni kweli tunakubaliana na gharama ya mchezaji mara nyingi inatokana na ubora wake, lakini hiyo haiwezi kuwa sababu ya kujiaminisha kwamba inaweza kuibeba Pyramids mbele ya Yanga.

Tulishuhudia msimu uliopita kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kelele kama hizo za wachambuzi na mashabiki wakiitoa Simba dhidi ya Al Ahly kabla na baada ya kuchezea kichapo cha mabao 5-0 nchini Misri.

Wengi walijiamisha kuwa Simba ingechezea tena kichapo nyumbani na imani hiyo ikiongezeka kutokana na Al Ahly kuwa wachezaji ghali huku ikielezwa kuna mmoja aliyenunuliwa kwa zaidi ya Sh. bilioni tano za Tanzania ukilingabisha na kikosi cha 'Wekundu wa Msimbazi' hao ambacho kikosi kizima kilikuwa cha Sh. bilioni moja tu.

Hata hivyo, Simba iliyokuwa ikitamba kwa kaulimbiu yao ya "Kila Mtu na Ashinde Nyumbani Kwao" ilifanya kweli na kuwachapa wanafainali hao wa Ligi ya Mabingwa Afrika wa msimu wa 2017/18.


Hivyo, hakuna kinachoshindikana kwa Yanga kufanya maajabu kama hayo ya Simba ama zaidi kama maandalizi ya kina, mipango na mikakati itafanyika kuelekea mechi hiyo huku ikipuuza kelele za wanaowabeza.

Yanga imekamilika idara zote kasoro tu safu ya ushambuliaji ndiyo inayohitaji kusukwa vema ili iweze kutumia vema nafasi inazopata, lakini timu hiyo ikipaswa kupata mechi nyingi za kirafiki ama kuzitumia hizi za Ligi Kuu ili kuwa na muunganiko mzuri.

Hilo likifanyika, hakika itazima kelele zote hizi ambazo Nipashe tunaziona ni sawa na kelele za chura ambazo siku zote haziwezi kumzuia tembo kunywa maji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Heko Bodi ya Ligi, viwanja vibovu vinaumiza wachezaji

Na Adam Fungamwango

**WIKI** iliyopita Bodi ya Ligi imevizuia viwanja vinne vya Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi Daraja la Kwanza kutokana na ubovu kwenye sehemu ya kuchezea.

Ofisa Mtendaji wa Bodi hiyo, Boniface Wambura, amevitaja viwanja hivyo kuwa ni Uwanja wa Kinesi uliopo Magomeni jijini Dar es Salaam na Bandari uliopo Temeke.

Viwanja hivi hutumika kwa Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara. Kwa upande wa Ligi Kuu, viwanja vilivyozuiwa ni Jamhuri Morogoro na Namfua uliopo Singida.

Wambura amesema wamevizuia viwanja hivi kutokana na ubovu kwenye eneo la kuchezea 'pitch' na kuagiza wahusika wawe wamerekebisha hali hiyo kabla ya mapumziko ya wiki ya mechi za kimataifa, yaani Kalenda ya Fifa kumalizika.

Akaongeza kuwa kama hali haitotengemaa basi wahusika watatakiwa watafute viwanja vingine mbadala hadi viwanja hivyo vitakaporekebishwa.

Ikumbwe kuwa Uwanja wa Jamhuri Morogoro unatumiwa na Mtibwa Sugar kama uwanja wake wa nyumbani, huku Singida United ikitumia Uwanja wa Namfua.

Hapa naona inaweza kuwa rahisi zaidi kwa Singida United, kwani inaweza kupeleka mechi zake kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, lakini tatizo linaweza kuwa ni kwa Mtibwa Sugar.

Timu hiyo inatumia uwanja huo mkubwa, baada ya uwanja wake wa Manungu kuondolewa kwenye orodha ya viwanja vinavyotumika Ligi Kuu msimu huu kutokana na kutokidhi viwango.

Niipongeze Bodi ya Ligi kwani uamuzi huu unaweza kufanya viwanja hivyo vikarekebishwa. Kwa muda mrefu wamiliki wa viwanja hivi wametakiwa kurekebishe viwanja hivi, lakini baadhi yao wameonekana kama vile kuziba pamba masikioni, hivyo kama vikizuiwa inaweza kabisa kuwafanya wakaharakisha marekebisho.

Hata Rais John Magufuli, Mei 19, mwaka jana, wakati akiwakabidhi Simba Kombe la Ubingwa wa Ligi Kuu kwenye Uwanja wa Taifa, aliwataka wahusika na wasimamizi wa viwanja vingi nchini ambavyo vinamilikiwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM), kuviboresha ili mpira uchezeke vizuri.

Kwa bahati nzuri kuna baadhi ya viwanja vinavyomilikiwa na CCM, vimeanza kukarabatiwa na kuwa vizuri na vyenye kuchezeka wakitii agizo hilo, mfano CCM Kirumba Mwanza na Samora Iringa, lakini baadhi kama vile Jamhuri na vingine ambayo havikutajwa bado havijafanyiwa matengenezo.

Viwanja vingi mikoani, pamoja na matatizo mengine, lakini ubovu mkubwa ni eneo la kuchezea ambapo wachezaji wamekuwa wakipata shida kuonyesha vipaji vyao, lakini kucheza kwenye mfumo ambao wamefundishwa na walimu wao.

Kutokana na hali hiyo ili kuendana na uwanja jinsi ulivyo, wachezaji wamekuwa wakibutua tu mipira kwa mtindo wa 'bora liende' na kusababisha hata mashabiki waikose burudani waliotaka kuiona baada ya kuingia uwanjani na pesa zao.

Nakumbuka kwenye mechi kati ya Mtibwa dhidi ya Mbeya City Septemba 29 kwenye Uwanja wa Jamhuri Morogoro, wenyeji Mtibwa walifungwa bao ambalo halikutokana na ubora wa Mbeya City au mchezaji, bali ubovu wa uwanja, kwani lilipigwa shuti dhaifu ambalo kipa Shaaban Kado alitarajia kulidaka, mpira ulidunda sehemu kwenye uwanja huo mkavu na usio na majani, ukapoteza uelekeo kabla ya kuingia wavuni.

Waliokuwa wanaangalia mechi hiyo kwenye televisheni walishangaa sana, na huenda ikawa hili limesababisha zaidi kuisukuma Bodi ya Ligi kuzuia viwanja vya aina hiyo.

Viwanja hivyo pia vinasababisha wachezaji wengi kuwa majeruhi mara kwa mara, hivyo kwa hili Bodi ya Ligi wanastahili sifa na ifike mahali sasa ligi ichezwe kwenye viwanja ambavyo wachezaji watafurahia kucheza, wanaoingia kwa viingilio watafurahia kuangalia kandanda safi la ufundi, lakini hata wanaoangalia kwenye televisheni nao kufurahia wanachokiona.

## KUMBUKUMBU MIAKA 20 KIFO CHA NYERERE

# WISIGANA NYERERE;
# Mbia wa Kambarage Butiama - Ikulu

**Na Mashaka Mgeta,** BUTIAMA

INGAWA si rahisi kumfananisha moja kwa moja na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, lakini zipo ishara na matendo ya utawala wa awamu ya tano chini ya Rais Dk. John Magufuli za 'kufuata nyayo' za mwasisi huyo wa uhuru wa Tanganyika na baadaye Tanzania.

Ndivyo anavyoamini Wisigana Nyerere (86), kaka pekee aliyebaki katika uzao wa Mtemi Nyerere Burito ambaye ni baba mzazi wa Mwalimu Nyerere.

Wisigana aliyezaliwa mwaka 1933 ni mtoto wa tisa kuzaliwa kutoka kwenye tumbo la Mugara Mutiro, mke wa nane kati ya wake 22 wa Mtemi Nyerere Burito.

Ingawa historia ya maisha yake na Mwalimu Nyerere (pichani) inatokea mbali, lakini Wisigana anasema ndiye aliyeongozana na Mwalimu Nyerere kutoka kijijini Butiama kwenda Pugu, alikokwenda kufundisha.

"Mwalimu Nyerere kwa vile alikuwa msomi na mimi niliishia darasa la tatu, alinichukua twende wote ili nikamsaidie kazi ndogo ndogo za nyumbani," anasema Wigisana anayejishughulisha na shughuli za kilimo na ufugaji kijijini Butiama.

Makazi yake yamepakana na mji wa awali wa Mwalimu Nyerere alioujenga wakati akishiriki shughuli za kutafuta uhuru, kabla ya kurejea kwenye makazi ya baba yake, Mtemi Nyerere Burito yanayojulikana kwa Kizanaki kama Mwitongo, maana yake ni mahame.

**KUJIUNGA TANU**

Wisigana anasema, baada ya kuwasili Pugu mwaka 1953, Mwalimu Nyerere alishiriki shughuli za kisiasa zilizolenga kudai uhuru, hivyo kujikuta akikabiliwa na ushindani mkubwa kutoka kwa wakoloni na baadhi ya Watanganyika (sasa Watanzania) walioanzisha upinzani dhidi yake.

Anasema haikuwa rahisi kumshauri Mwalimu Nyerere kuiepuka hatari iliyomkabili kwa kumtaka asiendelee na harakati za kudai uhuru, badala yake, yeye na wenzake waliendelea kumsaidia na kumtia moyo.

Wisigana anasema, mwaka 1954, TAA ilibadilika kuwa Tanganyika African Nation Union (TANU) na Mwalimu Nyerere aliendelea kuwa kiongozi wake.

Anasema ilipofika mwaka 1961, Tanganyika ilipata uhuru, yeye na dada zake wawili, Nyabhisenye na Nyakwe walikwenda kuishi Ikulu ya Magogoni jijini Dar es Salaam wakiwa na Mwalimu Nyerere aliyekuwa Waziri Mkuu na baadaye Rais wa Tanganyika (sasa Tanzania).


Wisigana anasema, baada ya kufika jijini humo, alipewa kazi ya kuwa mwangalizi wa mashamba ya serikali yaliyokuwa Mjimwema jijini Dar es Salaam na Iringa.

Anasema mwaka 1962, alirejea nyumbani kwake kijijini Butiama na kujishughulisha na kilimo na ufugaji, kazi zilizomfanya kuwa miongoni mwa wafanyabiashara wakubwa wa wakati huo.

Wisigana anasimulia licha ya maisha aliyoishi Ikulu, kurejea kwake kijijini hakukumsononesha kwa vile msingi wa maisha yake ulikuwa huko na kwamba hata Mwalimu Nyerere alikuwa anathamini maisha ya kijijini, licha ya kuwa kiongozi wa nchi.

Anasema kazi ya kwanza aliyoifanya ni kusimamia ujenzi wa nyumba ya Mwalimu Nyerere iliyopo eneo la ukoo wa Mtemi Nyerere, lililogawanywa kwa wana-ukoo akiwamo yeye (Wisigana).

Maneno hayo aliyotamka wakati wa uzinduzi wa makazi yake aliyojengewa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) eneo la Mwitongo, mahali yalipokuwa makazi ya baba yake, Mtemi Nyerere.



Wisigina ambaye kwa sasa ameteguka mguu, anaishi kwenye eneo hilo akiwa hana usaidizi kutoka kwa watu na taasisi zilizokuwa karibu na Mwalimu Nyerere.

**MWALIMU ALIUKABILI UPINZANI**

Wisigana anasema, moja ya mambo yaliyomweka Mwalimu Nyerere katika hatari na tishio la kukata tamaa ni vikwazo kutoka kwa wakoloni na upinzani kutoka kwa Watanganyika wazawa, akiwamo (jina tunalo) aliyewahi pia kuwa Katibu Mkuu wa TANU.

Anasema, ulikuwa wakati mgumu kwa vile, licha ya kuwapo vikwazo hivyo, haikuwezekana kumshawishi Mwalimu Nyerere aachane na harakati za kudai uhuru, badala yake wasaidizi wake akiwamo yeye (Wisigana) waliendelea kufuata maagizo yake.

Hata hivyo, anasema licha ya ushindani huo, Mwalimu Nyerere alijenga hoja kukabiliana na upinzani dhidi yake hadi kufanikisha kupatikana kwa uhuru.

**HULKA YAKE KIJIJINI**

Wisigana anasema wakati wa uhai, Mwalimu Nyerere alitenga muda wa kuishi na watu wa jamii yake katika kijiji cha Butiama, akiwa katika hulka na tabia zisizokuwa tofauti na anapokuwa katika majukumu yake ya kitaifa na kimataifa.

Anasema, yapo mambo mengi yaliyomchukiza hasa hongo zilizotawala kuanzia ngazi za chini kwenye jamii hadi kitaifa.

Pia Wisigana anasema hali ya kupenda ubinafsi na kujilimbikizia mali inayopaswa kutumika kwa maslahi ya watu wengi, ilikuwa miongoni mwa machukizo kwa Mwalimu Nyerere. Anasema, ufuatiliaji na hatua zinazochukuliwa na utawala wa Rais Dk. Magufuli hasa katika kudhibiti rushwa, matumizi mabaya ya madaraka na kudhibiti wizi dhidi ya mali za umma, vinaashiria 'kufuata nyayo' za Mwalimu Nyerere.

"Kwa hali ilivyo sasa tunaiona serikali inatumia mbinu za Mwalimu Nyerere na hali ikiendelea hivi, mambo mengi aliyokuwa akiyasimamia (Mwalimu Nyerere) yatarejea hata kama si kwa kiwango kile cha awamu ya kwanza," anasema.

**KUPENDA VIKAO**

Wisigana anasema jitihada zozote zinazofanywa kumuenzi Mwalimu Nyerere, zinapaswa kutoa kipaumbele kufanyika kwa vikao, ili kupata mawazo mapana zaidi yanayosaidia kufikia uamuzi sahihi kama alivyofanya (Mwalimu Nyerere).

"Viongozi wetu waendeleze utamaduni wa kukaa vikao, Mwalimu Nyerere alipenda sana vikao kuanzia kwenye ukoo wetu. Hata uamuzi aliokuwa anauchukua kwa sehemu kubwa ulitokana na majadiliano ya kwenye vikao," anasema.

**MAISHA YA KIDINI**

Wisigina anasema Mwalimu Nyerere alipenda dini hasa Kanisa Katoliki, hadi alipobatizwa kwenye misheni (hivi sasa ni parokia) ya Nyegina mkoani Mara mwaka 1953.

Anasema, mbali na Nyegena, misheni Katoliki nyingine zilizokuwapo kwenye ukanda huo ni Bumangi na Busegwe.

"Baada ya kuingia kwenye ukatoliki na kubatizwa jina la Julius, Mwalimu Nyerere alianza kufundisha dini kwa Wazanaki, ingawa hakueleweka kwa urahisi," anasema.

Anasema baada ya jitihada zake hizo, Mwalimu Nyerere aliamua kumleta Padri mmoja (ambaye hamkumbuki jina) kwenye misheni ya Magorombe iliyopo kijijini Butuguri na baadaye, akamwezesha ujenzi wa Kanisa Katoliki Parokia ya Butiama alipokuwa akisali.

Anasema, wakati Mwalimu Nyerere akijiwajibika katika kueneza dini kupitia kanisa Katoliki, Mtemi Edward Wanzagi alijiunga katika kanisa la Last Church of God. Wakati huo walikuwa wakisali chini ya mti.

Wisigana anasema, licha ya kuwa kwake karibu na Mwalimu Nyerere, yeye mwenyewe hakubatizwa, kwa vile baada ya kushiriki mafunzo na kufikia ukomo wa kubatizwa, Mwalimu Nyerere aliondoka Pugu kutokana na mgongano wa kisiasa uliokuwapo. "Nilishiriki mafundisho pale Pugu, lakini wakati nikikaribia kubatizwa, Mwalimu Nyerere, aliondoka na mimi nikaondoka, hivyo sikubatizwa hadi sasa," anasema.

**TAA NA TANU**

Wisigana anasema baada ya chama cha Tanganyika African Association (TAA) kubadilika kuwa Tanganyika African Nation Union (TANU), alikabidhiwa kadi namba 14, hivyo kuwa miongoni mwa walioshiriki kuandikisha wanachama wapya.

Anasema, uandikishaji huo ulikabiliwa na vitisho kutoka kwa wakoloni, hivyo kuwalazimu kujificha na wakati mwingine kuwaandikisha wanachama wapya kwa usiri mkubwa.

**SHANGWE ZA UHURU**

Wisigana anasema Desemba 9, 1961 akiwa kijijini Butiama, dunia ilitangaziwa uhuru wa Tanganyika, hivyo kusababisha shangwe kubwa maeneo mengi ya nchi, lakini zaidi kijijini Butiama.

"Tulikesha tukipiga na kucheza ngoma, tulikula na kunywa vyakula vya kitamaduni, tukafurahi sana kwamba kijana wetu ametimiza utabiri wa baba yake," anasema.

Kwa mujibu wa Wisigana, Mwalimu Nyerere alipaswa kuwa miongoni mwa Watemi, lakini baba yake, Mtemi Nyerere alikataa kwa sababu ya kuamini kwamba atakuwa na majukumu makubwa ya kitaifa.

"Mtemi Nyerere alisema Kambarage (Mwalimu Nyerere) hapaswi kuwa Mtemi kwa sababu utawala wake ni wa eneo dogo, lakini uwezo alionao utamfanya kuwa na majukumu kwa nchi nzima," anasema.


**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA (TMA)**

**MIAKA 20 KUMBUKIZI YA MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE**

**1999 – 2019**



Menejimenti na Wafanyakazi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) tunaungana na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli na watanzania wote katika kuadhimisha kumbukumbu ya kifo cha Muasisi wa Taifa letu na Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kilichotokea Octoba 14, 1999.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) tutaendelea kuyaenzi maisha yako kwa kutoa huduma bora za hali ya hewa.

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA
UBUNGO PLAZA, GHOROFA YA 3
S.L.P 3056
DAR ES SALAAM

SIMU: 255 (0) 22 2460706/7/8/
NUKUSHI: 255 (0) 22 2460735/2460700
BARUAPEPE:.met@meteo.go.tz/
TOVUTI:www.meteo.go.tz

# Serikali yakataza kufukuza wanafunzi karibia mitihani

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imepiga marufuku tabia ya baadhi ya shule hasa binafsi kufukuza wanafunzi kwa sababu ya utovu wa nidhamu kipindi wanapokaribia kufanya mitihani ya kitaifa.

Katazo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA), Dk. Charles Msonde, kwenye mahafali ya 15 ya Shule ya Msingi Tusiime ya Tabata jijini Dar es Salaam.

Alisema kuna waraka wa serikali unaoeleza adhabu inayostahili kuchukuliwa kwa mwanafunzi anayefanya makosa anapokaribia kumaliza shule badala ya kumfukuza shule moja kwa moja.

Dk. Msonde alisema kumfukuza shule hakumuumizi mwanafunzi pekee, bali ni maumivu makubwa kwa mzazi wake ambaye ametumia muda mrefu na gharama kubwa kumsomesha.

"Jiweke wewe kwenye nafasi ya mzazi, umemsomesha mtoto wako kuanzia awali anafika darasa la saba, kidato cha nne au cha sita anafukuzwa utajisikiaje?" Alihoji na kuendelea:

"Ni dhahiri kama ni mtoto wako utaumia, sasa kwanini shule isikae na mzazi wa mwanafunzi wakaona namna ya kumsaidia ili amalize salama."

Vile vile, alisema baadhi ya shule zimekuwa zikishikilia vyeti vya wanafunzi kama sehemu ya kuwashinikiza walipe ada au adhabu kwa wale watovu wa nidhamu, jambo ambalo alisema si sahihi.

Dk. Msonde aliwapongeza walimu na wamiliki wa shule hiyo, kwani imekuwa ikifanya vizuri kitaifa kwenye matokeo mbalimbali na hiyo imetokana na juhudi kubwa inayofanywa na walimu hao na mazingira mazuri yaliyopo.

"Ndugu zangu wazazi haya yaliyofanywa hapa na wanafunzi si mambo ya kawaida ni mambo ya ajabu sana, huwezi kuamini kwamba mwanafunzi wa darasa la tatu anaweza kusimama mbele za watu akajieleza kwa ufasaha kwa kujiamini tena kwa lugha ya Kiingereza."

"Mwingine amesoma hotuba ya Kiingereza kwa ufasaha, lakini aliyenivutia zaidi ni yule aliyekuwa akitafsiri maana alikuwa hasomi sehemu yoyote, lakini ametafsiri kwa ufasaha kwelikweli na naona watu wanaotafuta wakalimani huyo wa leo atawafaa," alisema Dk. Msonde.

Dk. Msonde aliyasema hayo baada ya kujionea shindano la wanafunzi hao wakijieleza kwa ufasaha na kwa ujasiri kuhusu umuhimu wa kujiamini kwenye maisha mbele ya wageni waliohudhuria mahafali hayo na mwingine kusoma hotuba ya Kiingereza kwa ufasaha huku mwenzake akitafsiri bila kusoma popote.

# Chadema yafunguka Lissu kurejea nchini

INATOKA UK. 2

kuwa ameshapona kabisa baada ya kukamilisha safari yake ndefu ya kimatibabu iliyoanza tangu Septemba 9 mwaka juzi jijini Dodoma na baadaye jijini Nairobi, Kenya na Ubelgiji alikokamilisha matibabu yake, hivyo kueleza kuwa sio sababu tena ya kuendelea kumuweka nje ya nchi.

Gazeti hili lilimtafuta Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) Simon Sirro, jana kuhusu madai ya Lissu na Chadema, lakini simu yake haikupokelewa.

Hata hivyo, akizungumzia kuhusu usalama wa mwanasheria huyo wa Chadema miezi mitano iliyopita, IGP Sirro alisema kukurejea kwa Lissu kutasaidia kukamilisha uchunguzi na kufahamu waliohusika na shambulio lake, na kwamba kama raia wengine wa Tanzania, anahakikishiwa usalama wake kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

"Kwanza tunashukuru kuwa amepona na sasa anarejea, tutaweza kufahamu zaidi waliohusika na shambulio lake, lakini pili usalama wake ni jambo la muhimu kama raia mwingine yeyote wa nchi hii ndio maana hata wewe upo salama kwa hiyo tutahakikisha anakuwa salama," Sirro alisema.

Awali Lissu alipanga kurejea nchini Septemba 9, mwaka huu siku ambayo mwaka 2017 alipigwa risasi 32 na watu wasiojulikana huku risasi 16 zikidaiwa kumpata mwilini, lakini baadaye aliahirisha kurudi kwa madai kuwa alikuwa hajamalizana na madaktari wake.

Hata hivyo Lissu aliahidi kuwa baada ya kuzungumza na madaktari wake Oktoba Mosi na Oktoba 8, mwaka huu angepanga tarehe nyingine ya kurejea nchini kabla ya kuahirisha tena wiki iliyopita safari hii akizungumzia hofu ya usalama wake.






# Mbarawa ateua sita

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, amewateua wakurugenzi watendaji sita wa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. Kitila Mkumbo, waziri huyo amemteua Mhandisi Ndele Mengo kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira j ijini Mbeya (Mbeya UWSSA) ambaye amechukua nafasi ya Mhandisi Simon Shauri aliyemaliza muda wake.

Alisema Mhandisi Mengo kabla ya kuteuliwa alikuwa Meneja wa Ufundi katika mamlaka hiyo.

Mwingine aliyeteuliwa katika uteuzi huo ni Mhandisi Aron Joseph ameteuliwa kuwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Moshi (MUWSA), ambaye amekuchukua nafasi ya Joyce Ally Msiru ambaye amemaliza muda wake na kabla ya uteuzi Mkurugenzi wa Idara ya Uzalishaji na Usambazaji Maji katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Dar es Salaam (DAWASA).

Pia Mhandisi Justine Rujomba ameteuliwa kuwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Arusha (AUWSA) ambapo amechukua nafasi ya Mhansiai Ruth Koya aliyemaliza muda wake. Rujomba alikuwa mhandisi katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Moshi (MUWSA).

Wengine walioteuliwa ni Mhandisi Leonard Msenyele ambaye ameteuliwa kuwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza (MWAUWSA). Anachukua nafasi ya Mhandisi Anthony Sanga aliyeteuliwa hivi karibuni kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji.

Alisema kabla ya uteuzi huo, Mhandisi Msenyele alikuwa Meneja wa Miradi katika Mamlaka hiyo.

# Siku 14 kubomoa nyumba mpakani

**Na Ibrahim Yassin,** SONGWE

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali, Nickodemus Mwangela, ametoa siku 21 kwa wakazi waliojenga maeneo ya mpaka wa Tanzania na Zambia wawe wamebomoa nyumba zao wenyewe na kuhama.

Agizo hilo linafuatia maelekezo ya Rais John Magufuli kuwataka watu hao wabomoe nyumba hizo na kuhama.

Rais Magufuli alitoa maelekezo hayo akiwa mkoani Songwe hivi karibuni kwenye ziara ya kikazi katika mji wa Tunduma akiwa na Rais wa Zambia, Edgar Lungu, wakati wakizindua kituo cha pamoja cha forodha.

Mkuu wa Mkoa akizungumza kwenye mkutano wa hadhara jana mjini Tunduma, alisema kutokana na agizo la Rais la kuachwa wazi eneo la mpaka huo linatakiwa lifuate ili eneo hilo liwe wazi, na kwamba hata kiongozi mwenzake upande wa Zambia naye anafanya mikutano akiwaeleza wananchi kuwa wahame ili eneo hilo liwe wazi kama walivyoelekeza. Alisema wakazi wa Tunduma wote ambao wamejenga kwenye mita 50 waondoke mapema kabla ya muda huo kufika kutokana na agizo ambalo limetolewa kutokana na umuhimu wa mpaka huo.

Alisema mwaka 2017 Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliagiza eneo la mpaka liwe wazi ambapo pia Mkuu wa Mkoa mtaafu, Chiku Galawa, alihamasisha watu wahame, lakini wananchi hawakutekeleza agizo hilo, jambo lililosababisha Rais Magufuli kuagiza tena akiwa na Rais Lungu ambaye naye aliwaagiza wananchi wake wabomoe.

# DC: Vinara wa migogoro ardhi wasichaguliwe uchaguzi mitaa

**Na Futuna Seleman,** RUFIJI

MKUU wa Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani, Juma Njwayo, amewataka wananchi wilayani humo kuchagua viongozi watakaoweza kuwasaidia kuleta maendeleo badala ya kuwachagua wanaochangia kuchochea migogoro hususan ya wafugaji na wakulima.

Amesema viongozi hao wamekuwa wakijinufaisha kwa migogoro hiyo.

Ameyasema hayo wakati akihamasisha uandikishaji wa daftari la wakazi kwa ajili ya kupiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaowahusisha viongozi wa mitaa, vitongoji na vijiji Novemba 24, mwaka huu.

"Msichague viongozi wanaoingiza ng'ombe usiku kwenye maeneo yenu, huku nyie mnagombana wenzenu wanakusanya fedha... wakati umefika wa kutowachagua viongozi hao, chagueni wanaoweza kuwasaidia kuwaletea maendeleo yenu, hiyo ndiyo dawa," alisema Njwayo. Aliwakumbusha wananchi hao kujitokeza kwa siku zilizobakia kujiandikisha kwa kuwa hiyo ndiyo nafasi pekee itakayomwezesha kila mwananchi kupiga kura.

"Nawaambieni ndugu zangu msijidanganye vitambulisho vya mpigakura haviruhusiwi kisheria... kajiandikisheni na nyie watendaji piteni nyumba hadi nyumba mashambani wafateni wananchi wajiandikishe kwa kuwa ni haki yao kupiga kura," alisema Njwayo.

Awali Kamanda wa Takukuru Wilaya ya Rufiji, Gwakisa Mwaikela, aliwataka wagombea kuepuka vitendo vya rushwa katika uchaguzi na wananchi nao kukataa kupokea rushwa kwa kuwa sheria itachukua mkondo wake.

"Chagueni viongozi watakaoweza kuwasaidia kuwaletea maendeleo, msikubali kupewa zawadi wala kitu chochote chenye kiashiria cha rushwa sheria itawabana, haitaangalia nani ni nani," alisema Gwakisa.

Baadhi ya wananchi walisema mwitikio mdogo wa kujiandikisha unatokana na baadhi ya wananchi kushinda mashambani na wengine kuishi maeneo ya mbali na vilipo vituo vya kujiandikisha, hivyo kuona shida kama wanapoteza muda kwenda kujiandikisha.




Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa Benki ya NMB, Donatus Richard, akimkabidhi mfanyabiashara Award Mpandila zawadi baada ya kuibuka mshindi wa safari ya kwenda China jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake wahimizwa kuchukua fomu

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

WANAWAKE mkoani Tabora wametakiwa kujitokeza kwa wingi kuchukua fomu za kugombea nafasi mbalimbali wakati wa uchaguzi ujao wa serikali za mitaa.

Wito huo ulitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, wakati akizungumza na wakazi wa Wilaya ya Sikonge wakati wa ukaguzi wa uandikishaji wa wananchi wenye sifa kwa ajili ya uchaguzi ujao.

"Fomu zitakapoanza kutolewa, jitokezeni kwa wingi ili mchukue fomu kwa ajili kuwania kuchaguliwa kuwa viongozi katika maeneo yenu mnayoishi," alisema.

Aidha, aliwataka wananchi ambao wameshajiandikisha kuhakikisha wanafanya maamuzi sahihi wakati wa kuwachagua viongozi wa ngazi za vitongoji, mitaa na vijiji. Mwanri alisema ni vema wakachagua viongozi ambao watakuwa mstari wa mbele kuwaletea maendeleo na ambao hawana kasoro.

Alisema endapo watafanya makosa katika uchaguzi huo, kijiji au mtaa husika utateseka kwa kipindi cha miaka mitano kutokana na kiongozi mbovu.

Katika hatua nyingine aliwataka wananchi wenye sifa ambao hawajiandikisha kutumia siku ya mwisho kuhakikisha wanajiorodhesha ili waweze kushiriki katika zoezi la kidemokrasia na kuwapata viongozi wawatakao.

Wakati huo huo, wakazi wa Mkoa wa Tabora ambao ni raia wametakiwa kuwafichua wageni ambao wanataka kujiandikisha na wengine kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi ujao wa serikali za mitaa.

Mwanri alisema serikali ilishaweka wazi kuwa watu ambao sio Watanzania wakiwamo wale wanaoishi katika Kambi ya Ulyankulu hawatashiriki uchaguzi huo kwa kujiandikisha wala kuomba kuchaguliwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi.

Mwanri alisema endapo itabainika kuna watu ambao sio Watanzania wamejiandikisha kinyume cha agizo la serikali, watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Katika hatua nyingine, amewatahadharisha viongozi wa asasi za kiraia na watu mbalimbali kutoka mataifa mbalimbali ambao wameomba kuwa waangalizi wa uchaguzi ujao katika mkoa huo kufanyakazi walioomba.

Alisema serikali haitasita kuwachukulia hatua kali wale wote ambao watafanyakazi nje ya ile ya uangalizi kama walivyoomba na kukubaliwa na serikali.

# Wanachama 10 Klabu Biashara waenda China

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA 10 wanachama wa Klabu za Biashara za Benki ya NMB (NMB Business Club), wameondoka nchini kwenda China, kushiriki maonyesho ya 125 ya Canton Fair 2019, yanayofanyika wiki hii mjini Guangzhou, ikiwa ni sehemu ya ziara yao ya kibiashara ya siku 10.

Akizungumza katika hafla ya kuwaaga wafanyabiashara hao kutoka kanda mbalimbali za klabu zao nchini, Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa NMB, Donatus Richard, aliwataka kuwa mabalozi wema wa NMB wakiwa China na kutumia vema elimu watakayopata kupitia maonyesho watakayoshiriki.

"Ni matumaini yetu kwamba mtaitumia vizuri safari hii kujifunza fursa mbalimbali za kibiashara zikiwamo za uwekezaji wa viwanda ili kuendana na kasi ya Tanzania ya Viwanda.

"Kufanya hivyo kutawasaidia kuongeza mbinu katika nyanja mbalimbali, ikiwamo kujua kwa namna gani mnaweza kushirikiana kufanya biashara kimataifa, hatua ambayo itawanyanyua kiuchumi," alisema Richard, huku akiwataka kurejea wakiwa bora zaidi kimbinu katika kukuza mitaji yao.

Donatus aliwasisitiza wafanyabiashara hao kuwa furaha ya benki hiyo kama taasisi kinara ya fedha nchini itakuwa ni kushuhudia mapinduzi chanya ya kimaendeleo kupitia elimu watakayopata kupitia ziara na maonyesho watakayoshiriki China.

Akitaja vigezo vilivyotumika kupata wafanyabiashara hao 10 kutoka miongoni mwa wanachama zaidi ya 200,000 kote nchini, Richard alisema ni pamoja na rekodi nzuri za marejesho ya mikopo na nguvu ya ushawishi ya mwanachama kuongeza wanachama/wateja wapya katika NMB.

Mwenyekiti wa NMB Business Club Wilaya ya Ilala, Award Mpandila, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kamuni ya Mpandilah General Supplies Ltd, aliishukuru benki hiyo kwa fursa waliyowapa, ambayo ana uhakika inaenda kubadili mifumo yao kibiashara.

Alibainisha ya kwamba, ziara ya siku 10, inayoambatana na ushiriki wa Maonyesho ya Canton Fair 2019, vitawaongezea elimu na kuwatia chachu ya mafanikio kibiashara na kwamba watarejea wakiwa wamejenga chaneli za ushirikiano na wafanyabiashara wa nchi hiyo.

"Ni fursa ambayo inatamaniwa na kila mtu aliye na kiu ya maendeleo," alisema Mpandilah.

# Serikali yatoa mil. 110/- matundu vyoo

**Na Hamisi Nasiri,** MTWARA

SERIKALI kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imeunga mkono kampeni ya ujenzi wa matundu ya vyoo 6,674 mkoani Mtwara kwa kuchangia Sh. milioni 110.

Kiasi hicho cha fedha kilitolewa jana mkoani Mtwara na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo iliyofanyika mkoani hapa na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali na binafsi.

Prof. Ndalichako alisema wizara imeamua kuunga mkono kampeni hiyo kwa kutoa fedha hizo kwa vile inatambua umuhimu wa wanafunzi kusoma wakiwa katika mazingira bora.

Alisema serikali itaendelea kuboresha mazingira katika sekta ya elimu ikiwamo miundombinu ya matundu ya vyoo, madarasa na nyumba za walimu katika shule zote nchini.

Prof. Ndalichako alisema dhamira ya serikali ni kuona sekta ya elimu nchini inakuwa na miundombinu bora, na wanafunzi hasa wa shule za msingi na sekondari wanapata taalumu wakiwa katika mazingira bora.

"Kupitia kampeni hii ya ujenzi wa matundu ya vyoo mkoani Mtwara, Wizara ya Elimu tunachangia Sh. milioni 110 ili kufanikisha lengo la kampeni hii," alisema Prof. Ndalichako.

Prof. Ndalichako ameridhishwa na kampeni hiyo inayolenga kutatua changamoto ya upungufu wa matundu ya vyoo na kueleza kuwa kila mdau kwa nafasi yake anapaswa kuunga mkono ili kila shule mkoani Mtwara iwe na choo bora.

Alisema sekta ya elimu ni muhimu kwa maendeleo ya nchi, hivyo mazingira bora ya kufundishia, kujifunzia pamoja na miundombinu ya matundu ya vyoo ni jambo la msingi kwa mwanafunzi ndio maana serikali imeunga mkono kwa asilimia 100 kampeni hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, aliishukuru serikali kwa kuunga mkono kampeni hiyo.

Alisema katika kampeni hiyo Mkoa wa Mtwara unahitaji kujenga jumla ya matundu ya vyoo 6,674 yenye thmani ya Sh. 6,674,000,000.

Alisema wadau mbalimbali mkoani humo wameshachangia zaidi ya Sh. milioni 50 na ahadi zikiendelea kutolewa.




Ofisa Masoko wa Kampuni ya Mars Communication Ltd, Wallu Amani (kulia), akikata keki na watoto wanaoishi katika kituo cha watoto wenye mahitaji cha Hisani wakati wa hafla ya kutimiza miaka 50 ya kampuni ya Hisense jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge abaini mwamko mdogo uandishaji S/Mitaa

**Na Mwandishi Wetu,** IGUNGA

MBUNGE wa Manonga, Seif Gulamali (CCM), amesema amebaini mwamko mdogo wa wananchi kujiandikisha kwa ajili ya kupiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliopangwa kufanyika mwezi ujao.

Gulamali aliyasema hayo juzi wakati akifunga mashindano ya michezo ya Kombe la Gulamali kwenye Uwanja wa Shule ya Msingi Nkinga wilayani Igunga mkoani Tabora.

Mashindano hayo ya mpira wa miguu na netiboli yalishirikisha shule za sekondari 16 kati ya 17 za Jimbo la Manonga.

Alisema amezunguka katika jimbo lake na kubaini kuwa tangu uandikishaji uanze Oktoba 8, mwaka huu, wananchi wengi jimboni kwake hawajajitokeza kujiandikisha ili waingizwe katika orodha ya wapigakura katika uchaguzi huo.

"Ninawakumbusha ndugu zangu wale wote wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea, twendeni tukajiandikishe kupiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

"Kile kitambulisho cha zamani cha mpigakura hakitasaidia kama huendi kujiandikisha sasa. Nenda kajiandikishe uchague kiongozi wako wa kitongoji na kijiji.

"Baada ya zoezi hili la uandikishaji wa wapigakura wa serikali za mitaa kumalizika Jumatatu, kutakuwa tena na uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura, tujitokeze pia kujiandikisha ili tupate haki yetu ya kumchagua diwani, mbunge na Rais. Nimeambiwa wengi hamjajiandikisha," alisema.

# Mamia wanafunzi wapewa taulo za kike

**Na Shaban Njia,** MBOGWE

ZAIDI ya wanafunzi wa kike 145 wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Masumbwe, Halmashauri ya Mbogwe mkoani Geita, wamepatiwa taulo za kike kama njia ya kuondokana na tatizo la ukosefu wa masomo wanapoingia katika siku zao za hedhi. Akikabidhi taulo hizo jana Mkuu wa Chuo cha Saint Joseph College Shinyanga, Miraji Zahoro Chomoka, alisema taulo zilizotolewa zitasaidia kuongeza ufaulu wa wanafunzi wa kike waliokuwa wakikosa masomo wakiwa kwenye hedhi.

Alisema, wanafunzi wakike wanaosoma katika shule za sekondari zilizopo pembezoni mwa miji wamekuwa wakikosa masomo na kufanya vibaya katika mitihani yao ya mwisho na wakati mwingine wamekuwa wakitumia vitambaa, magazeti, tishu au soksi ambavyo sio salama kiafya.

idha, Chomoka alisema tatizo la hedhi kwa wanafunzi wa kike limekuwa likisababisha wanafunzi kukosa masomo kwa siku 50 kwa kipindi cha mwaka mzima, hivyo kuporomosha ufaulu wao ukilinganisha na ufaulu wa wanafunzi wa kiume.

Makamu Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Zahara Abdallah, alisema shule hiyo ina jumla ya wanafunzi wa kike 908, huku kidato cha nne wakiwa 145, hivyo kuwa vigumu kila mmoja kumpatia taulo za kike.

Alisema wamekuwa wakinunua taulo za kike kupitia fungu la dawa baridi na wamekuwa wakiwagawia wanafunzi wa kike ambao hubainika wakati wameingia katika siku zao pindi wawapo shuleni au darasani.

Abdallah alisema ufaulu wa wanafunzi wa kike uko chini sana ukilinganisha na ufaulu wa wanafunzi wa kiume, na kwamba taulo zilizotolewa zitasaidia kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wa kike.

Naye Sabi Malima mwanafunzi wa kidato cha nne, alisema, wamekuwa wakikosa taulo za kike na wamekuwa wakikaa nyumbani hadi pale atakapomaliza siku zake za hedhi na akirudi shuleni anakuta wenzake wako mbele kimasomo.

# Amshukuru JPM huduma za afya

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

MHUDUMU wa afya na usafi wa mazingira katika Kituo cha afya Karume Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza, Ziada Ngwere, amempongeza Rais John Magufuli kwa jitihada za kuboresha huduma za afya nchini.

Mhudumu huyo ambaye taaluma yake ni mkunga wa jadi aliyeajiriwa na serikali mwaka 2011, kuwa mhudumu wa afya na usafi wa mazingira katika kituo hicho cha afya, Kata ya Shibula, ametoa pongezi hizo alipokuwa akizungumza na wanahabari.

Nampongeza Rais kuboresha huduma za afya nchini, ikiwamo zahanati, vituo vya afya, hospitali, vifaa vya kutolea huduma wagonjwa, miundombinu ya barabara pamoja na huduma za dawa, tofauti na zamani wagonjwa wengi walilazimika kukimbilia kwa waganga wa jadi na wakunga kupata huduma za matibabu alisema Ziada.

Ziada alisema kabla hajaajiriwa na serikali alikuwa akifanya kazi za ukunga tangu mwaka 1997 ambaye ameweza kuzalisha wajawazito zaidi ya 1,940 mtaani hadi mwaka huu na tangu aajiriwe katika Kituo cha Afya Karume ameweza kuzalisha kinamama zaidi ya 700.

Alisema kuwa pamoja na kuajiriwa na serikali, lakini bado wajawazito wanaendelea kwenda nyumbani kwake kupata huduma ya kujifungua hasa nyakati za usiku wanaposhindwa kwenda katika kituo cha afya kutokana na umbali wa zaidi ya kilomita mbili.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Karume, Dk. Samiah Nuru, alithibitisha mkunga huyo kuajiriwa na serikali kama mhudumu wa afya na usafi wa mazingira, na kuwa ni mchapakazi.





# Shule yakabidhiwa miradi ya maji

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

SHIRIKA la Kimataifa la Convoy of Hope nchini jana, limekabidhi miradi ya maji na umwagiliaji kwa Shule ya Msingi Ngaramtoni wilayani Arumeru na Mundarara wilayani Longido, ili waweze kulima kilimo cha hakika kwa ajili ya kuingizia kipato shule na kupata chakula cha mchana.

Akizungumza jana kwenye hafla fupi ya uzinduzi na makabidhiano ya miradi hiyo, iliyofanyika shuleni hapo, Mkurugenzi wa Shirika hilo nchini, Geofrey Mjema, alisema kuwa tangu shirika hilo lianze rasmi kufanya kazi mwaka 2013, limejikita katika kujengea uwezo shule kwa kuhamasisha programu za lishe shuleni kwa vitendo.

"Mradi huu wa majisafi na salama pamoja na mradi wa kilimo cha kisasa cha umwagiliaji umegharimu Sh. milioni 64 na lengo la kuiianzisha ili kuwezesha shule kulima vyakula vya kuingizia kipato au kununua chakula kwa wanafunzi pindi tutakapokoma kutoa ufadhili," alisema.

Alisema katika programu ya lishe shirika limefanikiwa kulisha zaidi ya wanafunzi 3,000 wa shule mbalimbali Arusha, ikiwa sehemu ya kupambana na utoro shuleni, kusaidia watoto kuelewa na kubaki shuleni jioni na kuwafanya watoto wawe na afya njema na kuwaepusha na maradhi.

Mjema alisema programu ya lishe shuleni ikiwamo Shule ya Msingi Ngaramtoni, ilianza mwaka 2013, wakati huo shule ikiwa na wanafunzi wachache wasiozidi 600 kutokana na ukosefu wa chakula.

Alisema kwa sasa shule ina wanafunzi zaidi ya 1,400 ambao wanapata mlo kamili wa mchana kwa siku tano za wiki.

"Mahudhurio ya wanafunzi yameongezeka kutoka asilimia 70 mpaka 98, zaidi sana ufaulu pia umeongezeka kutoka asilimia 65, mwaka 2014 mpaka sasa kufikia asilimia 95 kwa shule hii ya Ngaramtoni," alisema.

Alisema miradi hiyo kwa kushirikiana Shirika, serikali na kamati za shule, imegharimu zaidi ya Sh. milioni 110 kwa shule tano wanazohudumia ambazo ni Ngaramtoni, Lesing'ita, Mundarara, Emurutoto na Dympina ambayo ina kituo cha watoto wenye ulemavu wa viungo. Alisema lengo la Convoy of Hope kutoa fedha hizo ili kuona watoto wanasoma kwenye mazingira bora, huku walimu pia wakihudumia vizuri ili kujenga taifa bora la Tanzania.

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ngaramtoni, Twati Mollel, alilishukuru shirika hilo kwa msaada wa mradi wa kilimo cha umwagiliaji, mabanda ya kuku wa mayai, kisima cha majisafi, mabanda mawili ya kulima mboga (Green House), jiko la kisasa na kuwajengea maeneo ya kunawia mikono kwa ajili ya kuepukana na ugonjwa wa kipindupindu.

Aliomba shirika hilo kuendelea kuwasaidia kwa mwaka mmoja ili miradi ya umwagiliaji na kuku wao waweze kuwasaidia fedha za kumudu kununua chakula cha watoto na kuendelea kupata chakula bila kukatisha huduma hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, akiungumza katika hafla hiyo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, alilishukuru shirika hilo na kusema hayo ni matunda ya ushirikiano mzuri na serikali.



Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk Angeline Mabula, akiangalia moja ya majalada katika Ofisi za Ardhi Jiji la Mwanza jana, akiwa katika ziara yake ya kuangalia utendaji kazi katika sekta ya ardhi mikoa ya Kanda ya Ziwa. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Dk. Phillis Nyimbi.. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Watorosha mifugo kushtakiwa kwa uhujumu uchumi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

NAIBU Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega, amepiga marufuku wafugaji wenye tabia ya utoroshaji wa mifugo nje ya nchi, na kwamba wakigundulika watashtakiwa kwa makosa ya uhujumu uchumi.

Aliyasema hayo jana wakati akifunga semina ya uuzaji wa ng'ombe kwa kutumia mizani, iliyowashirikisha wafanyabiashara, wafugaji na wenyeviti wa vijiji, iliyofanyika katika mpaka wa Namanga.

Ulega alisema, wafugaji wengi wamekuwa na tabia ya kutorosha mifugo nje ya nchi kwa kisingizio cha soko na kuwataka kuuza mifugo hiyo nchini kwa kuwa sasa hivi mifugo yote inapimwa kwa kilo.

Alisema, wafugaji wengi wanapeleka mifugo yao nje ya nchi kutokana na uhakika wa soko kwa kuwa wananunua kwa kilo badala ya kukadiria.

"Mfugaji yeyote atakayepatikana akisafarisha mifugo nje ya nchi atashtakiwa kwa kosa la uhujumu uchumi na atapelekwa jela na hatajua atatoka lini, hivyo basi nawaomba sana mfuate sheria na taratibu za nchi," alisema Ulega.

Aliongeza kuwa, kitendo cha kutorosha mifugo nje ya nchi kinapelekea kuikosesha serikali mapato yake, na hivyo aliwataka kuuza mifugo yao nchini kwa kuwa sasa hivi inapimwa kwa kilo hali ambayo itamnufaisha mfugaji na kupata faida kubwa zaidi.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Longido, Jumaa Mhina, alisema, katika kudhibiti utoroshaji huo wa mifugo, wamejenga mnada mkubwa wa kisasa wilayani Longido ambao tayari umeanza kutumika na wafanyabiashara pamoja na wafugaji.

Uwepo wa mnada huo utawezesha wafugaji kupeleka mifugo yao na kupimwa kwa kilo badala ya kukadiria na mizani imeshapelekwa katika eneo hilo.

Mhina alisema kuwa hivi sasa mnada huo unapokea ng'ombe 300 kwa siku na mbuzi 2,000 na kwamba biashara ya kununua na kuuza mifugo katika eneo hilo ilishaanza, lakini changamoto bado ipo katika elimu jinsi ya kutumia mizani hiyo kwa wafugaji na wafanyabiashara hao, huku elimu zaidi ikiendelea kutolewa.

Naye Mmoja wa wafugaji Olesiada Sadala alisema kuwa, uwapo wa semina hiyo umewasaidia kujua matumizi sahihi ya mizani na umuhimu wa kufuata sheria na kanuni ikiwamo kulipia kodi.

Pia alisema kuanzishwa kwa mnada huo kumesaidia kutopitisha mifugo kwa njia za panya.

# Kampuni yazindua kifaa kufuatilia magari, pikipiki

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KAMPUNI ya Benson Arusha kwa kushirikiana na Afritrack, zimezindua programu ya kifaa cha ulinzi kitakachopachikwa kwenye vyombo vya moto na usafiri.

Teknolojia hiyo, itakuwa mahususi kwa ajili ya ufuatiliaji (Track) na kuviwekea ulinzi vyombo vya usafiri yakiwamo magari na pikipiki.

Akizungumza wakati wa kutambulisha programu hiyo, Ofisa Uhusiano kwa Wateja, Salma Rothbletz, alisema kifaa hicho, kitasaidia kuweka usalama wa vyombo vyote vya moto pindi vinavyokuwa barabarani.

Alisema lengo la kuletwa kwa huduma hiyo mkoani Arusha, imetokana na uhitaji mkubwa wa wateja kwa kuwa awali ilikuwa ikipatikana katika Mkoa wa Dar es Salaam pekee.

"Lengo la kuletwa kwa teknolojia hii Mkoa wa Arusha kila mara watu walikuja kwenye ofisi zetu wakitaka kufahamu sehemu vyombo vyao vya usafiri vilipo na vinafanya nini kwa wakati huo, pia wengine wamekuwa wakitaka tuwasaidie kutrack magari na pikipiki zao zilizoibiwa," alisema Salma.

"Kifaa hiki tunakifunga kwenye vyombo vyote vya moto, kina uwezo wa kuonyesha wapi chombo chako kipo kwa wakati huo na kinaunganishwa na simu yako ya mkono hivyo mhusika ataona kila kitu kinachoendelea kwenye gari au pikipiki yake," alisisitiza Salma.

Pia alisema teknolojia hiyo itapunguza matukio ya wizi wa magari na pikipiki kwa kuwa wamekuwa wakipokea malalamiko kutoka kwa wateja wao wakitaka kusaidiwa kupatikana kwa vitu walivyopoteza.

Aliongeza kuwa kifaa hicho gharama zake ni ndogo hata mwananchi wa kipato cha chini anaweza kuzimudu.

Meneja wa Kampuni ya Afritrack, Ashraf Mukri, alisema kampuni hiyo, inatoa huduma ya kuwaunganisha wateja na internet na kupokea taarifa kamili za vyombo vyao vya usafiri kwa wakati husika.

Ashraf alisema tofauti na teknolojia ya kufuatilia chombo cha moto kupitia mtandao, pia kampuni hiyo inatoa huduma ya kifaa kingine chenye uwezo wa kutoa taarifa kwa wateja endapo magari au pikipiki zao mafuta yapo au yamekwisha.

Alisema awali wakati wakitambulisha teknolojia hiyo, walikabiliwa na changamoto ya watu kutokuwa na elimu ya matumizi ya vifaa hivyo.

Vile vile, alisema lengo la kuanzishwa kwa progamu hiyo, ni kuwasaidia watu kupata huduma ya ulinzi na usalama wa vitu vyao.

Mkaguzi Msaidizi na Mtathmini wa Majanga ya Moto Mkoa wa Arusha, Lameck Kabagi, alisema progamu hiyo itakuwa na manufaa kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji hususani katika kitengo cha tahadhari na kinga ya moto.

# Watalii kutoka Israel wamiminika Moshi, Arusha

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MIJI ya kitalii ya Moshi na Arusha, imeanza kufurika idadi kubwa ya makundi ya watalii kutoka nchini Israel, baada ya serikali kupokea wageni hao zaidi ya 720 waliotua nchini kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

Mkurugenzi wa Bodi ya Utalii (TTB), Devotha Mdachi, akizungumza juzi usiku, wakati wa kuwapokea watalii hao alisema ujio wa wageni hao ni juhudi kubwa za utangazaji wa vivutio vilivyopo nchini uliofanywa na bodi hiyo kwa kushirikiana na balozi zake.

"Watalii hawa ni matokeo ya juhudi za utangazaji ambazo zimefanywa na Bodi ya Utalii Tanzania, lakini kwa kushirikiana na wadau kutoka sekta binafsi na ubalozi wa Tanzania nchini Israel. Hii ni ishara kwamba sasa soko la Israel limefunguka na tunategemea kwamba idadi ya watalii kutoka nchi ya Israel itaongezeka mara dufu," alisema.

Ndege nne zenye watalii kutoka nchini humo ziliwasili katika Uwanja wa Ndege Kimataifa wa KIA uliopo Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro juzi usiku, zikiwa na maelfu ya watalii.

Kwa mujibu wa TTB, watalii hao watapata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali zikiwamo hifadhi za taifa ili kujionea utajiri huo wa maliasili na baadaye waweze kwenda kushawishi watalii wengine katika nchi zao kuja kujionea wenyewe ni kwa jinsi gani Tanzania isivyosahaulika.

Kwa upande wake, Jaji mstaafu Thomas Mihayo, akizungumza baada ya ndege zilizowabeba watalii hao kuwasili alisema: "Niwaombe wote ambao wanahusika na mambo ya utalii wachukue maanani ya kwamba watalii ni lulu, kikubwa zaidi wawathamini. Na ndugu zangu sasa katika tasnia ya utalii wajifunze zaidi."

Idadi hiyo ya watalii kutoka nchi ya Israel imeongezeka nchini, hatua inayoifanya kutoka nchi ya 20 katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita hadi kuwa nchi ya sita kwa kiwango cha watalii wanaotembelea vivutio vya utalii ndani ya nchi.

# Mwarobaini changamoto za wasichana watajwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MPANGO wa kuwawezesha wasichana nchini Tanzania (GEP), kujitambua masuala ya hedhi salama, uwezeshaji wa kiuchumi, ukatili wa kijinsia na afya ya uzazi katika Wilaya ya Moshi, unatajwa ndiyo mwarobaini wa kumaliza usiri wa changamoto zao ikiwamo hedhi inayoendelea kuwafanya wengi wao kuwa gizani.

Mratibu wa Mpango huo, Immaculate Mworia, alisema ili watoto wa kike wawe na uwezo wa kushinda tamaduni yoyote yenye kikwazo, jamii na changamoto zinazoletwa na mwanadamu, vitu hivyo ni muhimu kwa sababu kuna mambo ambayo wazazi hawakuweza kupata nafasi ya kuzungumza nao.

"Tumetengeneza miongozo mbalimbali na hii inawalenga watoto wa sekondari na msingi. Ni miongozo ambayo watakuwa nayo watoto hawa na watakabidhiwa kupitia wawezeshaji wao ambao ni walimu; na kimsingi tumeanzisha klabu ambazo zitakuwa na wasichana 40 katika kila shule na watakuwa na hiyo miongozo.

"Inayo elimu kamilifu ambayo itawasaidia wasichana wawe na hamasa ya kujifahamu na kujitambua na kujijenga kwa maisha ya baadaye. Lakini pia wataelimisha na wengine ambao hawajapata nafasi ya kufikiwa na Kwieco katika shughuli zake."

Mpango huo wa mwaka mmoja unatekelezwa na Shirika la Kwieco, kwa ufadhili wa Taasisi ya Kimataifa ya Crossroads International katika kata tano za Mabogini, Mwika Kaskazini, Uru Kusini, Himo na Kibosho Kati.

Mworia ameeleza kuwa katika hedhi salama wamegundua kwamba wasichana wengi, bado wana ile hali ya kutojitambua kipindi gani anakuwa na hedhi, anajitunzaje akiwa katika hedhi na atumie nini kujitunza.

"Mabinti hawa tunaowazungumzia ni wale ambao bado hawawezi kununua vile visodo vya kuvaa (taulo za kike), hawana uwezo, kwa hiyo tunawafundisha namna ya kujitengenezea vitu vya kujihifadhi kama mabinti ili waweze kuendelea na shule, badala ya kukaa nyumbani," alieleza Mworia.

Akitoa maoni yake katika mjadala huo, Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Habiba Bomu, alisema mpango huo unaweza kuwa tiba ya changamoto hizo za wasichana, kwa sababu ukosefu wa elimu hufungua mlango wa safu kubwa ya taarifa za uongo na sintofahamu.

Mshauri wa Mpango wa Kuwawezesha Wasichana kutoka Taasisi ya Kimataifa ya Crossroads International, Magalie Menard alisema: "Nataka kujenga mahitaji ya usawa kuwa ya muhimu na kiujumla dunia haina namna ila kuyafanya haya kutokea.

Tabia zisizohitajika na za kumiza ambazo husababisha madhara ya kimwili, kiakili, kijamii na kiuchumi zinapaswa kuwa na mwisho. Nataka tufanye kazi pamoja ili kutokomeza ukatili wa kijinsia."

Hata hivyo, wakili maarufu na Mkurugenzi wa Shirika la Kwieco, Elizabeth Minde, akizungumza katika mjadala huo alieleza hisia zake kwamba hawawezi kuweka mwisho vitendo visivyohitajika bila kuwa na uwezo wa kuvitambua kwanza.

"Tunaamini elimu inaweza kutusaidia sisi kufikia maono yetu, kwa kuwafunza vijana wetu kuhusu masuala yanayoleta madhara kama vile ukatili wa kijinsia, tuna uwezo wa kujenga kikundi kikubwa cha jamii ambacho kitahakikisha haki sawa kwa watu wote. Mpango huu wa GEP umekuja kwa wakati sahihi," alisisitiza wakili Minde.



Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika Manispaa ya Moshi, Joyce Ndossi (aliyevaa nguo ya bluu), akizungumza jana na wadau kuhusu ujio wa mradi wa ujenzi wa nguvu ya pamoja ya kutetea wanawake na watoto kupambana na ukatili wa kijinsia. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Madiwani wahamishia ofisi Sekondari ya Kolila

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

NURU ya mafanikio iliyokuwa imezimwa na wakoloni kabla ya uhuru, imewaka tena kwa wananchi wa Old Moshi, baada ya Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, kufanya uamuzi mgumu wa kuzihamishia ofisi zake za utawala katika majengo ya iliyokuwa Shule ya Sekondari Kolila.

Shule ya Sekondari Kolila, ilifungwa zaidi ya miaka 10 iliyopita kutokana na kushindwa kujiendesha.

Uamuzi huo wa Halmashauri ya Moshi, kutengeneza historia mpya ya kupeleka ofisi zake ukanda huo wa juu wa milimani, uliandikwa mwishoni mwa wiki baada ya Mwenyekiti wa wake, Michael Kilawila, kutangaza uamuzi ulioridhiwa na kikao cha dharura cha Baraza la Madiwani.

Oktoba 7, mwaka huu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, aliagiza halmashauri 31 zenye ofisi nje ya maeneo yao ya utawala ikiwamo Halmashauri ya Moshi, kuhama katika kipindi kisichozidi siku 30.

Akizungumza katika kikao hicho, Kilawila alisema: "Ofisi za utawala za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, zitahamia eneo la lingine la utawala na tunatarajia kuhamisha ofisi za halmashauri yetu katika Shule ya Sekondari Kolila iliyopo Kijiji cha Tsuduni, Kata ya Moshi Mashariki."

Kilawila alisema mbali na kutii agizo hilo, pia watawasilisha ombi la kuongezewa muda wa mwaka mmoja ili kufanya marekebisho ya eneo hilo watakalohamia. Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Castori Msigala, alisema kamati ndogo iliyoundwa kuangalia maeneo ya kuhamia ilipendekeza kuhamia eneo hilo la Shule ya Sekondari Kolila.

Kwa mujibu wa Msigala, kuna gharama ndogo za kuhamia eneo hilo ikilinganishwa na kuhamia eneo la Mji Mdogo wa Himo, uliopo Njia Panda ya Moshi/Dar es Salaam. Waziri Jafo alieleza kuwa ametoa agizo hilo, baada ya kupokea maelekezo kutoka kwa Rais Dk. John Magufuli kuhusu halmashauri hizo. Alisema halmashauri itakayozembea kutekeleza agizo hilo itafutwa.

Halmashauri nyingine zinazotakiwa kufanya hivyo ni pamoja na Wilaya ya Arusha, Kondoa, Geita, Iringa, Mufindi, Bukoba, Mpanda, Kasulu, Kigoma, Moshi, Lindi, Babati, Mbulu, Musoma na Bunda. Nyingine ni Tarime, Mbeya Kilombero, Mtwara, Masasi, Newala, Njombe, Kibaha, Sumbawanga, Mbinga, Shinyanga, Bariadi, Singida, Nzega, Korogwe na Handeni.

Nipashe
# Spotika




ARSENAL YA EMERY IMEANZA KUIMARIKA? UK. 14



## ISIKUPITE

ENDAPO Cristiano Ronaldo atafunga bao leo wakati Ureno ikiivaa Ukraine ugenini kwenye mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020, atafikisha mabao 700 katika wasifu wake kisoka na hivyo kuwa mchezaji wa sita duniani kuweza kutimiza idadi hiyo ya mabao.



# WANGU WANGU...

Kiungo wa Hispania, Fabian Ruiz Pena (kushoto) akiwania kumiliki mpira dhidi ya kiungo wa Norway, Ole Selnæs kwenye mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 wakati timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1 nchini Norway juzi. HABARI UK. 30

SOKA



# ARSENAL YA EMERY IMEANZA KUIMARIKA?

**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal kwa sasa inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, ikiwa imepitwa pointi moja na Manchester City huku zote zikiwa zimecheza mechi nane.

Lakini je, nafasi hii kwenye msimamo wa Ligi Kuu inaonyesha kuimarika kwa kikosi hicho cha kocha, Unai Emery?

Ingawa ndio mwanzo kabisa wa msimu, lakini ukiiangalia Arsenal katika mechi zake za hivi karibuni za ligi, inaonyesha ishara tofauti kabisa.

Licha ya kuwa na rekodi nzuri ya kufunga mabao, mengi yakifungwa na mshambuliaji wake, Pierre-Emerick Aubameyang, kuruhusu nyavu zao kutikiswa ndio jambo ambalo linaonekana kuwa gumu zaidi kwa Arsenal wakiwa na rekodi ya kufungwa kwa asilimia 1.38 kwa kila mechi.

Usajili wa kipindi cha majira ya joto wa kumchukua beki wa kati, David Luiz kutoka Chelsea kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni nane bado hakujawa na mchango mkubwa, hasa kwa kutokuwapo kwa mabeki wa pembeni, Hector Bellerin na Kieran Tierney ambao wameumia na hilo linaifanya safu ya ulinzi ya Arsenal kuwa kwenye matatizo makubwa.

Matatizo ya safu ya ulinzi kwa kikosi cha Emery yanaonyesha kwamba, ni rahisi mno kwa kikosi hicho kuruhusu nyavu zao kutikiswa kirahisi.

Sare ya kufungana mabao 2-2 na Watford iliweka rekodi ya mashuti 31 kupigwa langoni mwa Arsenal, mchezo ambao kupata pointi moja ugenini yalikuwa matokeo bora zaidi kwa 'Washika Bunduki' hao.

Hata kama Arsenal inaweza kumaliza mchezo bila nyavu zake kutikiswa kama ilivyokuwa dhidi ya Bournemouth waliposhinda bao 1-0 nyumbani, lakini bado wanaonekana kuwa dhaifu.

Kumaliza mchezo bila kuruhusu nyavu zake kutikiswa, kunachukuliwa kama moja ya matokeo mazuri, lakini ikiwa bado safu yako ya ulinzi ikishindwa kuzuia mashambulizi ya mara kwa mara, inaonyesha wazi kwamba, kuna kazi ya ziada ya kufanya.

Arsenal mara zote inaonekana ni kama haijajipanga kwenye safu ya ulinzi na inakosa kiongozi. Kukosekana kwa fedha za usajili, si tena sababu kwa Emery.

Arsenal ilitumia kiasi kikubwa cha fedha kwa usajili ulioweka rekodi wa pauni milioni 72 kumsajili mshambuliaji, Nicolas Pepe peke yake.

Swali linakuja, kiasi hicho cha fedha si wangeweza kuwekeza kwa kuimarisha safu ya ulinzi? Kwani kwenye safu ya ushambuliaji Arsenal ilikuwa haina tatizo hilo.

Arsenal ya sasa ina safu ya washambuliaji vijana wakiwamo Joe Willock, Reiss Nelson na Gabriel Martinelli. Ingawa pia ilijaribu kuimarisha safu yake ya ulinzi kwa kuwasajili, Tierney, Luiz na William Saliba (ambaye alipelekwa kwa mkopo kule Saint-Etienne kwa msimu mmoja).

Nafasi ya Arsenal kwenye msimamo wa Ligi Kuu hiyo msimu huu inaonyesha ishara nzuri hasa kwa wapinzani wao Manchester United na Tottenham Hotspur, ambao ni kama wamekuwa kwenye wakati mgumu.

Spurs kwa sasa ipo nafasi ya 12 kwenye msimamo wa ligi hiyo, huku wapinzani wao wengine Chelsea wanaonekana kuwa kwenye kiwango cha kuridhisha wakiwa chini ya kocha, Frank Lampard.

Pamoja na kiwango chao bora, Arsenal imeshindwa kuwafunga Tottenham na United, wakiwa wametoka nyuma ya mabao 2-0 dhidi ya Spurs nyumbani.

Lakini pamoja na yote, kikosi cha Emery sasa kinakabiliwa na ushindani mpya wa kwenye nne bora, ambapo sasa wapinzani wao wanachomoza kuwa kikosi cha Brendan Rogers, Leicester City, ambao wamekuwa na matokeo yakuvutia zaidi msimu huu na hilo linaweza kuwa changamoto kubwa kwa Arsenal.

Uchaguzi wa kikosi cha Emery nao umekuwa ukizua maswali mengi, hasa kile alichokipanga dhidi ya United kwa kuichezesha timu kwa mtindo wa kupaki basi, huku Granit Xhaka, Matteo Guendouzi na Lucas Torreira wakianza.

Katika safu ya ulinzi walijikuta wakishindwa kutawala dimba, kutokana na kuwaacha nje viungo, Mesut Ozil na Dani Ceballos.

Uvumi umekuwa ukienea kwamba, Emery hamtaki Ozil na kwamba anataka kumuuza wakati wa kipindi cha dirisha dogo la usajili la Januari.

Hata hivyo, Emery bado ana kazi kubwa ya kufanya hapo Arsenal, na pengine wanaweza kuonyesha kuimarika zaidi kadiri msimu unavyozidi kuchanja mbuga.

JE, WAJUA?



MANCHESTER United imevuna pointi tisa tu kutokana na mechi nane za Ligi Kuu England hadi sasa msimu huu, idadi ambayo ni ya chini zaidi kuwahi kupata kwa idadi hiyo ya mechi za ligi tangu msimu wa 1989-90 (ilipovuna pointi nane tu kwa mechi hizo).

MICHEZO



Kikosi cha Pyramids

# PYRAMIDS KWA KUPINDUA MEZA KIBABE NDIO ZAO

**Na Adam Fungamwango**

DROO ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika na ile ya hatua ya mtoano ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyofanyika Jumatano iliyopita usiku jijini Cairo, Misri, imeipeleka timu ya Yanga ya Tanzania kucheza dhidi ya Pyramids ya nchini Misri.

Katika droo hiyo, Yanga imepangwa kuanza nyumbani Oktoba 27, kabla ya kwenda ugenini kwenye mechi ya marudiano Novemba 3, mwaka huu.

Hadi wakati huo, mashabiki wengi nchini hata ambao si wa Yanga, bado hawajaifahamu vizuri timu hiyo, ingawa wanaelewa kuwa timu za Misri kwa kawaida ni ngumu na zimekuwa zikifanya vema, zinapocheza na timu za Tanzania, hasa Yanga.

Baada ya hapo wengi wameandika kuhusu utajiri wa klabu hiyo, jinsi ilivyosajili wachezaji wake kwa gharama kubwa.

Kwenye makala haya, tutaiangazia timu hiyo jinsi gani ilivyopata nafasi ya kucheza Kombe la Shirikisho Afrika, ikicheza kwenye Ligi Kuu ya Misri msimu uliopita.

Tutaangalia kwa sasa ipo kwenye nafasi gani kwenye Ligi Kuu nchini humo, lakini pia ilifikaje hapo ilipo kwenye michuano hii hadi kufikia kupangwa na Yanga.

**Ipoteza mechi mbili tu msimu mzima.**

Pyramids ilianzishwa mwaka 2008, na ilianzia madaraja ya chini hadi 2014 ilipopanda Ligi Kuu nchini humo na ni timu iliyoleta mapinduzi makubwa kwenye soka la nchi hiyo, ikizitetemesha timu za Al Ahly na Zamalek ambazo zimekuwa zikilitawala soka la nchini humo.

Timu hiyo imepata nafasi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kumaliza Ligi Kuu Misri msimu wa 2018/19 ikiwa nafasi ya tatu kwenye msimamo.

Ilimaliza ikiwa imejikusanyia pointi 70 kwa kucheza mechi 34, ikishinda michezo 19, sare 13 na kufungwa mechi mbili tu. Zamalek ikimaliza nafasi ya pili kwa pointi 72 na bingwa ni Al Ahly kwa pointi 80.

Pyramids ndiyo timu pekee kwenye Ligi Kuu nchini humo msimu uliopita iliyopoteza mechi chache zaidi. Ilipoteza mechi mbili tu, huku Zamalek na Al Ahly zenyewe zikipoteza mechi nne kila moja.

**Inashika nafasi ya pili msimu huu**

Kwenye Ligi Kuu msimu huu, tayari imeshacheza mechi tatu na kushinda mbili, ikitoa sare moja, ikiwa kwenye nafasi ya pili nyuma ya Al Ahly, ikiwa na pointi saba.

Ilianza ligi kwa kishindo, ilipoichapa ENPPI mabao 4-0, mechi ya pili ikaifunga Tanta mabao 2-1, lakini kwenye mechi ya tatu ililazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Al Gaish.

Timu ya Al Ahly iko juu ya Pyramids kwa sababu imeshinda mechi zote tatu na kujikusanyia jumla ya pointi tisa.

**Ushindi ugenini ni kawaida yao**

Wakati Yanga ikiwa ina kaulimbiu yao ya kupindua meza kibabe ugenini, timu ya Pyramids inaonekana kuitekeleza vizuri zaidi kaulimbiu hiyo kwani inaonekana ni hatari zaidi ikicheza ugenini.

Katika michuano ya Kombe la Shirikisho, inaonekana kupindua meza ikiwa ugenini.

Mechi yake ya raundi ya awali ilianzia nyumbani dhidi ya Etoile du Congo ya nchini Congo Brazzaville na kuinyuka mabao 4-1.

Kama vile haitoshi ikaenda ugenini nchini Congo na kuinyuka tena timu hiyo bao 1-0.

Ikatinga raundi ya kwanza ya michuano hiyo na ikacheza mechi yake ya kwanza nyumbani dhidi ya CR Belouzdad na kulazimishwa sare ya bao 1-1, lakini ikaenda kupindua meza ugenini kwa kushinda bao 1-0, hivyo ikasonga mbele kwa jumla ya mabao 2-1.

Ushindi huo ndiyo umeipa nafasi timu hiyo kucheza na Yanga iliyoanzia Ligi ya Mabingwa, iliyoitoa Township Rollers kwa jumla ya mabao 2-1, ikitoka sare ya bao 1-1 nyumbani na kushinda ugenini bao 1-0 kabla ya kutolewa na Zesco kwa jumla ya mabao 3-2, baada ya sare ya bao 1-1 nyumbani na kufungwa mabao 2-1 ugenini na kuangukia kwenye mechi hiyo ya mchujo ya Kombe la Shirikisho kusaka nafasi ya kutinga hatua ya makundi.

## NJE YA UWANJA

Steve Bruce amefikisha mechi ya 400 kufanya kazi ya ukocha Ligi Kuu England wakati alipoiongoza Newcastle dhidi ya Man United, hivyo kuwa kocha wa saba kuweza kutimiza idadi hiyo kwenye ligi hiyo. Lakini pia ni kocha wa nne kuweza kushinda katika mechi yake ya 400 kwenye michuano hiyo (wengine walioweza kufanya hivyo ni David Moyes, Alex Ferguson na Arsene Wenger).



## Extra Time



LIVERPOOL

# KLABU 4 ZILIZOKWEPA MATOBO LIGI 5 ULAYA

**LONDON, England**

MSIMU mpya wa Ligi Kuu za Ulaya umeanza kwa staili yake na ya kuvutia. Umetoa burudani, mshtuko, mshangao na maumivu kwa baadhi ya klabu.

Klabu nyingine tangu kuanza kwa Ligi hiyo, hazijaonja uchungu wa kufungwa ['kutobolewa'] hadi sasa na hapa tuziangalia klabu nne kutoka kwenye ligi kubwa tano-bora Ulaya ambazo bado hazijaonja machungu ya kufungwa.

Ushindi na vipigo vinabakia kuwa sehemu ya mchezo wa soka. Timu nyingi zimezifanya zile pinzani kuwa na wakati mgumu.

Makala haya yanazichambua klabu nne kutoka katika ligi tano kubwa Ulaya ambazo hadi sasa, bado hazijafungwa...

**4. Wolfsburg**

Umekuwa mwenendo wa kushangaza kwa VFL Wolfsburg msimu huu, wameonyesha ushindani mkubwa kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga. Baada ya msimu uliopita kumaliza katika nafasi ya sita kwenye msimamo, Woflsburg imerudi kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani msimu huu ikiwa na nguvu kubwa zaidi.

Ni moja kati ya klabu nne katika ligi tano za Ulaya ambayo hajapokea kipigo kwenye Ligi Kuu. Wolfsburg ilianza msimu kwa ushindi wa 2-1 dhidi ya FC Köln. Tangu hapo imekuwa imara siku hadi siku.

Wolfsburg kwa sasa ipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Bundesliga ikiwa na pointi 15, baada ya kupata ushindi mara nne na sare tatu kwenye mechi zake saba. Kama itaweza kuendelea kuwa katika kiwango hicho, basi inakuwa na msimu bora zaidi kwa upande wao.

**3. Real Madrid**

Real Madrid ilikumbana na wakati mgumu wa kukatisha tamaa kwenye mashindano yote iliyoshiriki msimu uliopita. Los Blancos hao walishindwa kuwika mbele ya Julen Lopetegui na Santiago Solari, na hata kurudi kwa Zinedine Zidane hakuweza kuwazuia kumaliza msimu kwa matokeo mabovu.

Miamba hiyo ya Hispania iliamua kuingia sokoni ili kuimarisha kikosi chake wakati wa kipindi cha usajili. Ilitumia euro milioni 300 kuwasajili wachezaji kama Eden Hazard, Eder Militao, Rodrygo, Ferland Mendy na Takefusa Kubo kutua hapo kwenye dimba la Santiago Bernabeu. Wakati uwekezaji wao ukiwa bado haujazaa matunda mazuri kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, hali yao kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, ni ya kuvutia.

'Los Blancos' hao kwa sasa wapo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu wakiwa na pointi 18 katika mechi 8 walizocheza msimu huu. Rekodi yao ya ushindi mara tano na sare tatu kutoka mechi nane zinaifanya kuwa moja ya klabu chache barani Ulaya ambayo haijakumbana na kipigo msimu huu barani Ulaya.

2. Juventus

Hawa ni miamba wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Juventus wamemwonyesha kila mmoja kwamba kwa nini waliamua kuachana na kocha wao wa zamani Massimiliano Allegri na kumchukua Mtaliano mwingine, Maurizio Sarri. Wakati malengo yao makubwa msimu huu ni kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwenye ligi ya nyumbani msimu huu wameonyesha kuwa bora zaidi.

Licha ya kwamba msimu huu Ligi ya Serie A inaonyesha kuwa na ushindani mkubwa, 'Bianconeri' hao wameanza msimu vizuri zaidi. Baada ya ushindi wa 2-1 dhidi ya Inter Milan, mabingwa hao watetezi sasa wapo kileleni mwa msimamo wakiwa na pointi 19.

Vijana hao wa Sarri sasa wameshinda mechi sita na kutoka sare moja kati ya saba walizocheza kwenye Ligi Kuu ya Italia msimu huu. Pia wamefunga mabao 13 na kuruhusu nyavu zao kutikiswa mara sita tu.

**1. Liverpool**

Liverpool ilipitwa kwa pointi moja tu kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu dhidi ya Manchester City. Hata hivyo, Wekundu hao wameonyesha ishara ya kutorudi nyuma, kwani wameendelea na kasi ya kuufukuzia ubingwa huo msimu huu.

Vijana hao wa Jurgen Klopp wameonyesha kuwa hawazuiliki kwenye mbio za ubingwa huo. Wameshinda mechi zote nane kwenye Ligi Kuu hadi sasa, wakifunga mabao 20 na kuruhusu kufungwa mabao sita tu hadi sasa. Kwa sasa wanaongoza msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 24 katika mechi nane juu ya Man City, ambao wapo nafasi ya pili na pointi zao 16.

Wekundu hao wanapanga kuweka rekodi kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu. Kwa kile wanachokionyesha hadi sasa, unaweza kuwa msimu bora zaidi kwa kikosi hicho cha pale Merseyside.

## Nukuu


"Ninampenda mchezaji [Pepe] na ninadhani ulikuwa uamuzi mzuri wa [kumsajili], bado hajamaliza kuzoea vizuri, unapaswa kumpa muda kidogo. Kwa sasa anaonekana kidogo kutocheza kwa uhuru kama alivyokuwa akifanya akiwa Ufaransa. Kwa upande mwingine, lazima niseme tunao wachezaji makinda wazuri ambao wanaweza kucheza pembeni, [na] hilo atapaswa kupigania nafasi," **Kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger akizungumza na Omnisport.**



"Romelu [Lukaku] ni mchezaji ambaye ni lazima ajifue zaidi, kwa sababu mwili wake unahitaji mazoezi zaidi kupata uwiano mzuri, kujifua, kucheza na kuwa kwenye mwili mzuri. Huu ndio mwanzo wa msimu, alikuwa na matatizo ya mgongo na sasa anatakiwa kujifua zaidi," **Kocha wa Inter Milan, Antonio Conte**



"Madrid ndio ni pazuri. Ndio, walikuwa na majeruhi wengi, lakini sihuzuniki kwa kutokuwa pale, nina furaha kubwa hapa Arsenal, nimecheza mechi 11, ambapo nimeonyesha ubora wangu na sasa nipo pale nilipotaka kuwapo," **Kiungo wa Real Madrid, Dani Ceballos anayeichezea Arsenal kwa mkopo akiwaambia waandishi wa habari akiwa na kikosi cha timu ya Taifa ya Hispania wiki iliyopita.**



## Michezo



Kikosi cha Yanga

# YANGA YA KIRUMBA IKIISUBIRI PYRAMIDS

**Na Adam Fungamwangwo**

MECHI ya Kombe la Shirikisho la Soka Afrika kati ya wawakilishi pekee nchini, Yanga na Pyramids ya Misri itachezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza.

Viongozi wa Yanga wameeleza sababu mbalimbali za kiufundi na kisaikolojia kuipeleka mechi hiyo mjini Mwanza, lakini ukweli unabaki pale pale kuwa mechi hiyo ya mkondo wa kwanza ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, itachezwa Oktoba 27, mwaka huu kwenye uwanja huo.

Hii haitakuwa mara ya kwanza kwa mechi za kimataifa kuchezwa kwenye uwanja huo kwani mwaka 1987, Simba ilicheza dhidi ya Al Ahly ya Misri katika Uwanja wa CCM Kirumba kwenye michuano hiyo ya Kombe la Shirikisho, wakati huo ikiitwa Kombe la Washindi Barani Afrika.

Katika mechi hiyo ya raundi ya pili kama hii, Simba ilishinda mabao 2-1 yaliyofungwa na Zamoyoni Mogella na Mtemi Ramadhani, bao la kufutia machozi la wageni likifungwa na mchezaji bora wa Afrika kwa mwaka huo, Mohamed Al Khatib 'Bibo'.

Simba ilitolewa baada ya kufungwa mabao 2-0 ugenini, lakini Al Ahly hiyo hiyo ndiyo iliyotwaa kombe hilo mwaka huo.

Kwa maana hiyo Uwanja wa CCM Kirumba, si mgeni kuchezewa michuano hiyo. Kwenye makala haya tutaangalia mechi tano za nyuma ambazo Yanga imecheza uwanjani hapo na matokeo yake.

Kwa ufupi ni kwamba rekodi zinaonyesha kuwa kwenye uwanja huo, Yanga haina matokeo mazuri sana, wala mabaya sana.

Kwa mechi saba ambazo Yanga imecheza kwenye uwanja huo, imeshinda mechi tatu, kufungwa tatu, ikitoka sare moja, lakini baada ya mechi hiyo ya sare ilishinda kwa mikwaju ya penalti.

**1. Yanga 2-0 Toto African**

Tunaanza na mechi za Yanga katika Uwanja wa CCM Kirumba kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2016/17, ambapo Oktoba 19 ilicheza mechi yake dhidi ya Toto African na kushinda mabao 2-0.

Mabao ya washindi katika mechi hiyo yalifungwa na Obrey Chirwa dakika ya 28 na Simon Msuva kabla hajauzwa nchini Morocco, alikifunga bao hilo kwa mkwaju wa penalti dakika ya 55.

**2. Yanga 0-1 Mbao FC**

Mechi hii ilikuwa ni ya nusu fainali Kombe la FA kusaka bingwa atakayeiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, iliyochezwa Aprili 30, 2017, kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza, Yanga ikicheza dhidi ya Mbao FC.

Yanga ikiwa ndiyo mabingwa watetezi wa kombe hilo, ilivuliwa ubingwa kwa kufungwa bao 1-0. Bao pekee kwenye mechi hiyo lilikuwa la kujifunga, Andrew Vicent 'Dante', akijifunga mwenyewe dakika ya 27, akiwa katika harakati za kuokoa krosi iliyopigwa na Pius Buswita ambaye msimu huo alikuwa akiichezea Mbao FC.

Mbao ilikwenda fainali na ikafungwa mabao 2-1 na Simba kwenye mechi ya fainali mjini Dodoma.

**3. Yanga 0-1 Mbao FC**

Yanga ilirejea tena kwenye Uwanja wa CCM Kirumba mwezi uliofuata kucheza na timu hiyo hiyo ya Mbao FC. Safari hii ilikuwa ni kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2016/17. Ilikuwa ni Mei 20, 2017.

Mambo yakawa ni yale yale, Yanga ikaambuliwa kipigo cha bao 1-0, ingawa hakikuiathiri timu hiyo kutwaa ubingwa na Tanzania Bara.

Bao la Mbao FC lilifungwa na straika wao hatari wakati huo, Habib Haji Kyombo.

**4. Yanga 0-2 Mbao FC**

Msimu uliofuata wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2017/18, Yanga ilikwenda kwenye Uwanja wa CCM Kirumba kucheza dhidi ya Mbao FC, lakini kwa mara nyingine tena ikaambulia kipigo. Safari hii kilikuwa cha mabao 2-0.

Mechi hiyo ilichezwa Desemba 31, 2017, ikiwa katika harakati ya kutafuta kuutetea ubingwa wake. Alikuwa tena ni Habib Haji Kyombo aliyefunga mabao yote mawili dakika ya 53 na 68 na kuuweka ubingwa rehani ambao msimu huo ukachukuliwa na watani wao wa jadi, Simba.

5. Yanga 2-1 Mbao FC

Yanga ilianza kupata matokeo mazuri kwenye Uwanja wa CCM Kirumba mwaka huu, ilipolipiza kisasi kwa kuifunga Mbao FC mabao 2-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita, 2018/19.

Ilikuwa ni Februari 20, mwaka huu, ilipofanya hivyo, mechi hiyo ikaitwa ni ya kuvunja mwiko. Mbao ilianza kupata bao dakika ya 45 kupitia kwa Ndaki Robert.

Dakika ya 50, Yanga ilisawazisha lililofungwa na Heritier Makambo, kabla ya Amissi Tambwe kufunga bao la ushindi kwa mkwaju wa penalti, ikatoka na ushindi wa mabao 2-1.

**6. Yanga 1-0 Alliance FC**

Ilikuwa ni Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita 2018/19 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Machi 2 mwaka huu, Yanga ikicheza na timu iliyopanda Ligi Kuu msimu huo, Alliance FC.

Katika mechi hiyo, Yanga ilishinda bao 1-0, lililowekwa wavuni na Tambwe dakika ya 75 na kuifanya timu yake kuongeza idadi ya mechi za kushinda kwenye uwanja huo.

**7. Yanga 1-1 Alliance FC (penalti 4-3)**

Hii ilikuwa ni mechi ya Kombe la FA iliyochezwa Machi 30 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba na timu hiyo hiyo ya Alliance FC.

Katika mechi hiyo, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1 dakika 90 za mchezo, kabla ya Yanga kushinda mechi hiyo kwa mikwaju ya penalti 4-3.


Dakika ya 38, Makambo alifunga bao na kuipatia Yanga bao la kuongoza, kabla ya Joseph Jemes kusawazisha dakika ya 62.

Penalti za Yanga ziliwekwa wavuni na Paul Geofrey, Thabani Kamusoko, Haruna Moshi na Deus Kaseke, huku penalti za Mrisho Ngassa na Kelvin Yondani zikiota mbawa.

Kwa upande wa Alliance penalti zake zilifungwa na James Joseph, Geofrey Luseke na Sameer Vicent, huku Martin Kiggi, Dickson Ambundo, na Siraji Juma wakikosa penalti zao, shujaa wa Yanga akiwa ni kipa Klaus Kindoki akiokoa penalti mbili.

Hiyo ndiyo ilikuwa ni mechi ya mwisho ya Yanga kucheza kwenye uwanja huo, huku kwa hivi karibuni kukiwa hakuna mechi ya kimataifa iliyocheza kwenye dimba hilo.

## NAJUA WAJUA



KINDA Newcastle, Matty Longstaff amekuwa mchezaji wa pili kinda zaidi (miaka 19 na siku 199) kuweza kufunga bao la ushindi dhidi ya Manchester United kwenye Ligi Kuu England, baada ya Jermain Defoe (aliyefanya hivyo dhidi ya West Ham, Desemba 2001 akiwa na miaka 19 na siku 62).

## SOKA



# MAJI HAYA ATAYAOGA SOLSKJAER MAN UTD

Pogba

**MANCHESTER, England**

NI msimu mwingine ambao makocha walioshindwa kuzisaidia timu zao kuvuka viwango fulani wamepata shinikizo kali kutoka kwa bodi simamizi za timu wanazozinoa mbali na mashabiki wa timu hizo.

Shinikizo katika baadhi ya timu zimesababisha kufutiliwa mbali kwa makocha hao ama hata kupewa onyo la kufutwa iwapo misururu ya matokeo mabaya itaendelea kushuhudiwa.

Majuzi Klabu ya AC Milan ilimteua Stefano Pioli kama kocha wake mpya, baada ya kufukuzwa kwa Marco Giampaolo Jumanne iliyopita baada ya miezi mitatu.

Hatua hiyo ilichukuliwa baada ya msururu mbaya wa matokeo. Lakini si timu hiyo pekee ambapo kocha wake alikabiliwa na shinikizo kali na hatimaye kufutwa kazi.

Klabu ya Olympique Lyon ya Ufaransa ilimfuta kazi kocha wake, Sylvinho baada ya kuwa na matokeo mabovu kutoka walipompa kazi miezi michache iliyopita.

Ingawa makocha kama vile Zinedine Zidane wa Real Madrid, Mauricio Pochettino wa Tottenham na Marcos Silva wa Everton pia wapo chini ya shinikizo kutokana na matokeo mabaya.

Katika klabu ya Everton, aliyekuwa kocha wa timu hiyo, David Moyes anapigiwa upatu kuchukua nafasi ya Silva, huku Jose Mourinho akitarajiwa kumrithi Zinedine Zidane iwapo atapigwa chini.

Silva huenda akaachishwa kazi baada ya timu yake kushindwa kupata ushindi wa ligi tangu siku ya kwanza ya Septemba licha ya kununua wachezaji wapya.

Klabu hiyo ilimuunga mkono na zaidi ya pauni milioni 100 msimu uliokwisha, lakini kumekuwa na ishara chache za timu hiyo kuimarika uwanjani.

Mourinho ni miongoni mwa makocha waliokumbwa na kipindi kigumu katika klabu ya Man United kutokana na matokeo mabaya yanayodaiwa kusababishwa na mbinu yake ya uchezaji, uhusiano mbaya kati yake na wasimamizi wa bodi ya timu hiyo pamoja na wachezaji na kadhalika.

Ni nini kilichojiri? Alipigwa shoka na nafasi yake kuchukuliwa na Ole Gunnar Solskjaer ambaye ni mmojawapo wa wachezaji wa kikosi cha United kilichoshinda Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2009.

Baada ya kocha huyo kuanza na mguu mzuri, kwa kushinda mechi 14 kati ya 19 akiwa kaimu, alisaini mkataba wa miaka mitatu.

Lakini tangu hapo kocha huyo ameshindwa kuinoa timu hiyo licha ya kupewa fursa ya kusajili wachezaji wakati wa dirisha la uhamisho lililopita.

Na kufikia sasa timu hiyo ipo katika nafasi ya 12 na pointi tisa baada ya kucheza mechi nane huku ikishinda mara mbili kushindwa mara tatu na kutoka sare mara tatu.

Wachambuzi wanatabiri kwamba timu hiyo itajikuta katika eneo la kushushwa daraja baada ya mechi dhidi ya Liverpool na Norwich hatua ambayo huenda ikaamua hatima ya kocha Ole Gunnar Solskjaer.

Matumaini pekee ya United kujizolea pointi ni kucheza katika Uwanja wa Old Trafford, lakini hilo pia halijaizuia United kupoteza mechi.

Kocha huyo ameshinda mechi mbili pekee kati ya 13 na hivyo kuwa mara ya kwanza kwa United kuanza vibaya katika Ligi Kuu England katika kipindi cha miaka 30.

Amedaiwa kuwaambia wachezaji wake kwamba kazi yake ipo hatarini baada ya klabu hiyo kushindwa na Newcastle mbali na kuwasisitizia wachezaji hao kwamba hatima zao hazijulikani iwapo hawataimarika.

"Ningependa kuomba msamaha kwa mashabiki kwa sababu hatushindi mechi, lakini hilo litatokana na kuanza upya kujijenga, hivyo tumejipatia jukumu kubwa la kuweza kufaulu katika timu sita bora, bila kujali timu nne bora. Hivi sasa tunahitaji matokeo ili tuweze kwenda mbele," alinukuliwa akisema.

**ANAHITAJI MUDA?**

Kocha huyo amekuwa akiomba kupewa muda zaidi na usimamizi wa timu hiyo kuwa na subira naye. Licha ya kuwanunua Harry Maguire, Aaron wan Bissaka pamoja na Dan James bado mambo yanakuwa magumu.

Ukweli ni kwamba wachezaji hao watatu wameanza vema ni suala ambalo limemshawishi Makamu Mwenyekiti Mtendaji, Ed Woodward kuwa klabu hiyo ipo katika mwelekeo mwema.

Tatizo ni kwamba Woodward na Man United wataendelea kulimbikiziwa lawama iwapo watahisi kuendelea kumuunga mkono Solskjaer.

Hata hivyo, baada ya kuruka kutoka kocha mmoja hadi mwingine tangu alipostaafu Sir Alex Furguson kuna kiu ya kuwa na kocha mpya ambaye ataendelea kuinoa timu hiyo.

**NDANI YA 18**



MABAO 10 kati ya 12 ya David Luiz kwenye Ligi Kuu England, amefunga akiwa uwanja wa nyumbani, na la mwisho ni aliloifungia Arsenal kwa mara ya kwanza wakati ikicheza dhidi ya Bournemouth kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa.



MSIMU mpya wa Ligi Kuu za Ulaya umeanza kwa staili yake na ya kuvutia. Umetoa burudani, mshtuko, mshangao na maumivu kwa baadhi ya klabu. Klabu nyingine tangu kuanza kwa Ligi hiyo, hazijaonja uchungu...

**Uk. 16-17**



# SABABU 4 RONALDO KUIPA JUVE UEFA

**TURIN, Italia**

NI msimu mwingine na ukurasa mpya umeanza kwa mchezaji mwenye historia ya kipekee kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Cristiano Ronaldo.

Wote wanajua kwamba, wakati wake akiwa pale Real Madrid alikuwa na rekodi yake katika mashindano hayo. Na tangu ameondoka pale Santiago Bernabeu amekuwa akiwania kulibeba taji hilo na hivi sasa akiwa na timu nyingine kabisa.

Juventus waliamua kumchukua Ronaldo ili kuipata ile rekodi aliyokuwa nayo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kwamba walikuwa na imani kubwa mafanikio aliyoyapata kule Real yanaweza kutua hapo Turin.

Msimu uliopita mambo hayakwenda kama yalivyopangwa. Si kwamba CR7 hakutoa mchango wake uliotakiwa, lakini tu mambo yalikuwa tofauti na matarajio.

Ronaldo alifanya kazi kubwa kuhakikisha mafanikio ya kule kwenye dimba la Bernabeu yanatua hapo kwa 'Kibibi Kizee' hicho, lakini jitihada zake hazikuzaa matunda.

Lakini sasa msimu mpya umeanza na vitu vingi vinaipa nafasi klabu hiyo ya Turin msimu huu kuwa na nafasi kubwa ya kufanya kweli.

Huu unaweza kuwa msimu ambao Ronaldo atatengeneza historia na heshima kubwa na kuthibitisha kwa nini yeye ni mchezaji bora katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Makala haya yanakuchambulia sababu nne kwa nini Mreno huyo anaweza kuipata taji la michuano huyo Juventus msimu huu:

**4. Kuweka historia yake**

Wote tunajua kwamba Ronaldo hana aibu ya kuonyesha majukumu yake, na Juve iliiambia dunia kwa nini waliamua kumnunua ili kuwaongoza kwenye mafanikio ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Itachukuliwa kama pande mbili zizoshindwa pamoja, kama Juve haitafikia mafanikio hayo.

Jambo muhimu zaidi, utakuwa ni wakati wa CR7 kutimiza malengo yake katika kipindi chake cha uchezaji. Ni wazi kwamba mazungumzo yote yatakuwa: Alibeba wakati akiwa United na Real, lakini ameshindwa akiwa Juve.

Ronaldo hatataka kuharibu wasifu wake. Kwamba kwa sasa malengo yake ni kukabiliana na changamoto iliyopo mbele yake.

Inajulikana wazi kwamba, Ronaldo akishakiweka kitu chake moyoni, ni lazima akikamilishe na hakuna wa kumzuia. Mashabiki wake watakuwa na matumaini makubwa ya kuona anatimiza malengo yake na kuiongoza Juventus kwenye ndoto za kubeba taji hilo.

**3. Messi kubeba tuzo ya Fifa**

Si siri kwamba, kumekuwa na ushindani mkubwa baina ya wachezaji hawa wawili bora zaidi kuwahi kutokea katika zama hizi - Ronaldo na Lionel Messi. Kama mmoja kati ya wawili hao anapata tuzo binafsi, mwingine naye atapigana kuhakikisha naye anaibeba pia.

Hadi mwezi uliopita, walikuwa wameshinda mara tano kila mmoja tuzo ya Ballon d'Or na ile ya mwanasoka bora wa mwaka wa Fifa. Hata hivyo, Messi aliongeza tuzo nyingine ya mchezaji bora wa mwaka wa Fifa na kumzidi Ronaldo ambaye kwa vyovyote atataka naye kuibeba.

Njia ipi bora ya kushinda tuzo hiyo kubwa? Na heshima gani kubwa zaidi ya kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya?

Ronaldo anajua kwamba, ili kupata tuzo nyingine, ni lazima abebe taji la Ulaya. Na hilo litamlazimu kufanya kila kitu ndani ya uwezo wake kuhakikisha analibeba taji hilo.

**2. Ushawishi wa Maurizio Sarri**

Bianconeri wanajulikana kwa kuwa na safu imara ya ulinzi isiyopitika, na hilo ni tofauti na staili aliyokuwa nayo kocha wa mwanzo, Massimiliano Allegri. Na hilo lilikuwa na athari kwa kiwango cha Ronaldo msimu uliopita.

Kwa ujio wa Maurizio Sarri na safu yake ya ushambuliaji ikiwa na mbinu mpya, Ronaldo atakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kufunga mabao tofauti na ilivyokuwa msimu uliopita.

Wakati wa kipindi cha Ronaldo pale Real, kipindi ambacho hakuwa kwenye fomu nzuri zaidi ni wakati akiwa chini ya kocha, Jose Mourinho.

**1. Juve ina kikosi bora msimu huu**

Ni ukweli uliowazi kabisa kwamba, Juve wana kikosi bora zaidi msimu huu kuliko msimu uliopita. Ingawa walikuwa bora katika msimu uliopita, Bianconeri hao sasa wameongeza nguvu zaidi kwenye timu yao, hasa baada ya kufanya usajili wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Kibibi Kizee hicho cha Turin kimeimarisha zaidi safu yake ya ulinzi kwa kumsajili Matthijs de Ligt kutoka Ajax. 'Dogo' huyo mwenye umri wa miaka 20, bila shaka yoyote ni mmoja wa walinzi bora zaidi vijana barani Ulaya kwa sasa. Tayari ameanza kuzoea maisha ya soka la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kwa kuonyesha kiwango cha kuvutia kabisa hadi sasa.

Wachezaji kama Gianluigi Buffon, Gonzalo Higuain na Leonardo Bonucci wote wamerudi kikosini hapo, huku wachezaji kama Danilo na Luca Pellegrini pia wapo kwenye uwanja huo wa Allianz kwa ajili ya kuiimarisha zaidi timu hiyo.

Ingawa Ronaldo ataongoza mashambulizi, sapoti ya wachezaji hawa itafanya kazi kuwa rahisi zaidi.

**USILOLIJUA**

Arsenal imeshinda jumla ya mechi 17 za Ligi Kuu England katika uwanja wake wa nyumbani chini ya kocha Unai Emery tangu kuanza kwa msimu uliopita, ni Liverpool (21) na Man City (20) tu ambazo zimeshinda mechi za nyumbani zaidi yake kwenye EPL.



# Uharibifu miundombinu majitaka walalamikiwa

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya, imelalamikia matumizi mabaya ya miundombinu ya mtandao wa majitaka katika Jiji la Mbeya.

Imesema wamekuwa wakikuta miili ya watoto wachanga, watu wazima na taka nyingine ngumu kama nguo, kwenye mabomba ya majitaka.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Ndele Mengo, wakati akizungumza na maofisa watendaji wa kata na mitaa ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Aliwaomba kushirikiana na mamlaka hiyo kutoa elimu kwa wananchi na kufichua vitendo vya uharibifu na uhalifu vinavyofanyika kwenye miundombinu ya maji kwenye maeneo yao.

"Uharibifu na uhalifu kwenye mazingira ya vyanzo vya maji unasababisha majitaka kuvuja na kusambaa mitaani, hali ambayo inahatarisha afya na maisha ya wananchi," alisema Mengo.

Alisema watendaji wa kata na mitaa jijini Mbeya wanakazi ya kutoa elimu kuhakikisha wananchi wanatunza vyanzo vya maji ili kuepukana na magonjwa ya milipuko, lakini pia ukame.

Baadhi ya maofisa hao watendaji wameitaka mamlaka hiyo, kuchukua hatua za haraka pale wanapotoa taarifa za majitaka kuwapo kwa chemba za majitaka zinazovuja ili zisilete madhara kwa wananchi hasa wa mabondeni.

Mmoja wao, Upendo Mtenzi Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Mbalizi Road, alisema tahadhari hiyo itasaidia wananchi wanaoishi mabondeni kuepukana na magonjwa ya milipuko kama kipindupindu endapo chemba hizo zitaachwa ziendelee kuvuja.

Mwenyekiti wa maofisa watendaji wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Jumanne Mwasenga, alisema wataendelea kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya miundombinu ya majitaka pamoja na kuikumbusha mamlaka wajibu wake pale wanapoona hali ya miundombinu hiyo sio nzuri.



Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Tanga, Solomon Mwangamilo, akiwafafanulia wananchi na abiria waliokwama katika daraja la Jitengeni Kata ya Segera mpakani kati ya Handeni na Korogwe. Zaidi ya abiria 1,000 wamekwama kusafiri. **PICHA: BONIFACE GIDEON.**

# Maofisa ugani wadaiwa kuwatelekeza wakulima

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

WAKULIMA wa Kijiji cha Kilambo katika Kata ya Mwatenga, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, wamewalalamikia maofisa ugani wakidai hawawatembelei mashambani kutoa elimu ya kilimo bora, hali inayosababisha wasizalishe kwa tija.

Walisema kuwa katika maeneo yao walishauriwa kutumia kilimo cha umwagiliaji, lakini kutokana na maofisa hao kutotoa elimu ya kutosha kwao, wanashindwa kukitumia vizuri.

Wakizungumza na Nipashe, wakulima hao walisema kuwa licha ya serikali kuwaagiza maofisa ugani kuwatembelea wakulima kutoa elimu na ushauri, lakini bado hawafanyi hivyo na wanaona matamko ya serikali kama hayana maana.

Mmoja wa wakulima hao, Benard Nsimbe, alieleza kuwa amekuwa akijishughulisha na kilimo kwa zaidi ya miaka 20 katika eneo hilo, lakini hajawahi kuona ofisa ugani kuwatembelea kutoa elimu na kwamba analima kilimo cha mazoea.

Alisema wanatumia nguvu kubwa na uwekezaji katika kilimo cha mpunga, lakini mavuno wanayopata ni duni, hali ambayo inawakatisha tamaa kwani hawapati ushauri wa kitaalamu.

"Hakuna maofisa ugani hapa kwetu, watu tumelima enzi za Tanganyika, tumevuna enzi za Tanganyika yawezekana ndio maana wanatudharau, wanashinda tu kwenye ofisi za halmashauri inasikitisha," alisema Nsimba. Aliongeza kuwa wanatambua umuhimu wa kuwa na maofisa ugani ndani ya jamii, na kwamba kitendo cha kutowatembelea wakulima kinarudisha nyuma jitihada za kulima kilimo bora kitakachomnufaisha mkulima.

Hata hivyo walieleza hofu katika mifugo yako kuwa haipatiwi chanjo kwa wakati na wakati mwingine kufa.

Waliongeza kuwa ni mara chache hufika kutoa chanjo, lakini na mifugo yao imeendelea kufa. Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Rueben Mfune, mara kwa mara amekuwa akiwaagiza maofisa ugani kuwatembelea wakulima katika maeneo yao ili kutoa elimu ya kilimo bora badala ya kushinda ofisini.

Mfune aliwahimiza kazi zao za ugani wakazifanye kwa wakulima ili wapate maarifa na ujuzi wa namna ya kulima kilimo chenye tija.

# Watishwa magonjwa ya mlipuko

**Na Grace Mwakalinga,** MBOZI

WAKAZI wa Mtaa wa Mbugani katika Kata ya Ichenjezya, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, wamesema wapo hatarini kupata magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu na kuhara kwa madai kuwa dampo la kuhifadhia taka limewekwa karibu na makazi yao.

Walidai kuwa licha ya dampo hilo kuwekwa karibu na makazi yao, pia taka hizo zimekuwa zikirundikwa muda mrefu bila kuzolewa na mamlaka husika.

Wakizungumza juzi na Nipashe, wananchi wa mtaa huo walieleza kuwa ni mwezi mmoja umepita tangu taka zirundikwe bila kuondolewa katika dampo hilo, na kwamba wakati mwingine hulazimika kuzichoma moto, hali ambayo huwasababishia moshi na harufu mbaya.

Miongoni mwa wananchi hao, Justina Ngole, alieleza kuwa dampo la taka lipo mita tano kutoka kwenye makazi yake, hivyo anakerwa na harufu inayotoka kwenye taka hizo, na kuongeza kuwa mara kwa mara watoto wake wamekuwa wakiugua matumbo na kifua.

"Hili ghuba (dampo) la taka linanisababishia kero kubwa kwa sababu watu wanatupa mizoga na kuchoma taka za plastiki ambazo harufu yake ni mbaya, na inaweza ikanisababishia madhara kiafya," alisema Ngole.

Mwenyekiti wa Mtaa huo, Nelson Kaminyoge, alisema suala hilo amelipeleka kwenye uongozi wa Halmashauri ya Mji wa Vwawa, na kwamba mpaka sasa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa, ikiwamo kuliondoa dampo au kuzoa taka.

Mwenyekiti huyo alibainisha kwamba kuna madampo mawili katika mtaa huo, na kwamba njia inayotumika ni kuchoma moto, huku akieleza hofu kwa watoto kupata magonjwa ya milipuko na kukanyaga moto.

"Nimefikisha suala hili kwenye uongozi wa Halmashauri ya Mji wa Vwawa lakini mpaka sasa hakuna utekelezaji wowote, nadhani hili jambo limekaaa kisiasa, hofu yangu ni wananchi kupata madhara kwa sababu ya uchafu huo," alisema Kaminyoge.

Akitolea ufafanuzi wa suala hilo, Ofisa Usafi wa Mazingira Halmashauri ya Wilaya hiyo, Hamis Nzunda, alisema tatizo la taka katika mtaa huo linafahamika na wameanza kuchukua hatua za kuziondoa, ingawa hakusema ni lini.





# Watanzania waaswa matumizi ya dawa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WANANCHI wameshauriwa kuacha tabia ya kutumia dawa bila ushauri wa wataalamu wa afya ili kujiepusha na madhara yatokanayo na matumizi holela ya dawa.

Hayo yalielezwa na kiongozi wa timu ya madaktari bingwa, Dk. Nassoro Mzee, alipokuwa na waandishi wa habari kwenye matibabu ya kibingwa yaliyotolewa katika Viwanja vya Msikiti wa Nughe, jijini hapa.

Dk. Mzee alisema matumizi holela ya dawa hizo yanasababisha kujenga usugu wa magonjwa.

"Hizi dawa zinaponya, lakini pia ni sumu matumizi yake yanatakiwa kuzingatia ushauri wa wataalamu wa afya hivyo matumizi holela yanaweza kusababisha madhara au kifo hivyo wanatakiwa kuchukua tahadhari hiyo," alisema.

Alisema wananchi wanatakiwa kumwona mtaalamu wa afya ili kuchukuliwa vipimo na kujua aina ya ugonjwa unaomsumbua na ndipo wataweza kuandikiwa aina ya dawa za kutumia.

"Kwa kawaida ugonjwa wowote unapoingia kwenye mwili wa mtu lazima utasikia homa, lakini aina ya ugonjwa itaonekana kwa njia ya vipimo hivyo tusitumie dawa kabla ya kufika hospitali kumwona daktari akupe ushauri," alisema.

Kuhusu huduma hiyo, Mtaalamu huyo alibainisha kuwa timu hiyo ilikuwa ikitoa huduma matibabu ya kibingwa bure kwa wananchi, lakini dawa zilinunuliwa na uongozi wa msikiti huo na kutoa bure kwa wagonjwa.

Aliongeza kuwa katika kambi hiyo walibaini magonjwa mengi yanayowasumbua wagonjwa waliofika kwao kuwa ni shinikizo la damu, uzito uliopitiliza na kinamama wengi kusumbuliwa na tatizo la hedhi.

Mmoja wa wagonjwa, Suleman Mruta aliomba matibabu hayo kuwa endelevu na kushukuru timu ya madaktari hao kuona umuhimu wa kutoa matibabu bure wananchi.

"Kama mnavyojua gharama ya matibabu ni kubwa leo hii tumeweza kukutana na madaktari hawa jambo ambalo ukienda Hospitali ya Mkoa au Benjamini Mkapa kuwaona ni gharama, lakini leo tumehudumiwa bure," alisema.

Kwa upande wake, Imamu wa Msikiti wa Sunni Nughe, Shekhe Abdalah Juma, alisema kilichowasukuma kuomba kutoa huduma za afya hapo ni kutokana na gharama za matibabu kuwa kubwa na wakati mwingine baadhi ya watu hushindwa kumudu.

Shekhe Juma alisema katika siku hiyo wananchi walichangia lita zaidi ya 100 za damu na watu zaidi ya 200 walifika katika kambi hiyo kupata huduma za kiafya.

Alisema matibabu hayo yalishirikisha wananchi wote bila kujali itikadi ya dini na yatakuwa endelevu kutokana na mwitikio wa watu wengi.



Muuguzi Bahati Charokiwa (kulia), akimpima shinikizo la damu Hawa Steven mkazi wa Mkonze jijini Dodoma jana, wakati wa matibabu ya kibingwa yaliyotolewa bure na madaktari kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kwa kuombwa na uongozi wa Msikiti wa Sunni Nughe. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# AMCOS zatakiwa kuanzisha Saccos

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika nchini imewaagiza wakulima wa ushirika wa mazao (AMCOS) kuanzisha Ushirika wa Akiba na Mikopo (Saccos) ili ziweze kuwasaidia kujikwamua kiuchumi wakati wa msimu wa mavuno. Akizungumza jana na Nipashe, Kaimu Mrajisi wa Tume hiyo, Edmund Masawe, alisema wakulima wanatakiwa kuwa na Saccos zao ambazo zitawasaidia kukopeshana na kujiwekea akiba kabla ya msimu wa kuuza mazao.

Alisema wakulima wengi wanalazimika kuuza mazao yao kwa hasara ili kukidhi mahitaji yao kutokana na kutokuwa na fedha.

"Tunaomba AMCOS zote jitahidini kuanzisha Saccos zenu lengo ni kutaka kuona mnanufaika na kilimo mnachofanya na si vinginevyo," alisema Masawe.

Alifafanua zaidi ya kuwa Tume hiyo inahitaji kuona wana AMCOS wote wanapiga hatua katika kilimo wanachofanya na si kutoa malalamiko. Alisema Tume imejipanga kuanza kutoa elimu kwa jamii kuhusu ushirika wanachofanya kutokana na watu kutojua nini maana ya ushirika.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Utafiti na Mafunzo wa Tume hiyo, Dorothy Kalikamo, alisema wataendelea kutoa mafunzo kwa kila wanaushirika ambao watakuwa wameanzisha ushirika kwa ajili ya kufanya maendeleo.

Dorothy alisema hivi sasa taifa linaelekea katika uchumi wa kati wa viwanda, hivyo ni vema kila mmoja akajua nafasi yake katika kazi anayofanya ili kujiinua kiuchumi. Alisema wakulima na wafugaji wote wanapaswa kufanya vitu hivyo kwa tija na hakuna sababu ya wananchi kuendesha vitu vyao kiholela bila kuanzisha ushirika.

# ALAT yataka Watanzania kuenzi demokrasia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JUMUIYA ya Tawala za Mitaa nchini (ALAT), imewataka Watanzania kuzingatia misingi ya demokrasia iliyoasisiwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 24, mwaka huu.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Elirehema Kaaya, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uandikishaji wa daftari la orodha ya wapigakura wa serikali za mitaa.

Alisema uchaguzi huo mwaka huu unaenda sambamba na maadhimisho ya miaka 20 ya kifo cha Baba wa Taifa ambaye alikuwa muumini mkubwa wa demokrasia.

"Zoezi hili linakwenda sambamba na maadhimisho ya miaka 20 ya kifo cha baba wa Taifa niwakumbushe Watanzania, Mwalimu Nyerere alikuwa ni muumini mkubwa wa demokrasia, lakini alikuwa muumini mkubwa wa haki, alipinga rushwa kwa nguvu zake zote," alisema.

Pia alisema Baba wa Taifa aliasisi misingi mizuri ya demokrasia na alichukia rushwa na kuwataka kujiepusha na vitendo hivyo wakati wa uchaguzi huo.

"Mwalimu alisema walipogundua mtu amepokea au kutoa rushwa hawakuachia mahakama peke yake, walihakikisha mtu huyu anapata viboko 12 wakati anaingia na 12 wakati anatoka ili akamwonyeshe mkewe, jambo la kumchapa mtu mzima sio jambo dogo, lakini Baba wa Taifa alijaribu kuonyesha ni jinsi gani anavyoichukia rushwa," alisema.

Alitoa rai kwa viongozi wote na Watanzania kuheshimu na kumuenzi Baba wa Taifa kwa kupiga vita rushwa, umaskini, ujinga na maradhi.

Aliwahimiza wananchi wenye sifa watakaokuwa wamejiandikisha kwenye daftari hilo, wachukue fomu kwa ajili ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Kaaya aliwataka wananchi kujiepusha na vitendo vya ubaguzi wa kijinsia, kidini, rangi na ubaguzi wa namna yoyote katika uchaguzi huo ili kupata viongozi bora.





# Masheha waombwa kusaidia vita dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kati, Hamida Mussa Khamis, amewataka masheha wa ukanda wa pwani na wakuu wa madiko (sehemu za uvuvi), kuisaidia serikali katika kuendeleza mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Akizungumzia marekebisho ya sheria mpya ya dawa za kulevya kwa masheha wa ukanda wa pwani, wakuu wa madiko na maofisa wa kikosi cha kuzuwia magendo (KMKM) katika ukumbi wa halmashauri ya wilaya hiyo Dunga, alisema licha ya serikali kuchukua juhudi ya kuzifanyia marekebisho sheria ya dawa za kulevya, bado tatizo hilo linaendelea kuiathiri jamii.

Alisema ni vyema masheha na watendaji hao kuacha kuona aibu, badala yake kuwafichua na kuwaripoti waingizaji na wasambazaji wa bidhaa hizo ili waweze kuchukuliwa hatua.

Alieleza kwamba kufanya hivyo kutasaidia kupunguza ama kutokomeza kabisa vitendo hivyo nchini.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya Zanzibar, Kheriyangu Mgeni Khamis, alisema tangu kufanyiwa marekebisho sheria hiyo na kuanza kutumika, kuna mafanikio kadhaa yameanza kupatikana.

Akiyataja mafanikio hayo, alisema ni pamoja na kutiwa hatiani kwa baadhi ya watendaji wa vitendo hivyo na kutumikia adhabu ya kifungo kulingana na makosa yao.

Washiriki wa kikao hicho waliishauri tume hiyo kunyimwa dhamana kwa watuhumiwa wa vitendo hivyo pamoja na kuweka vituo maalum katika maeneo yenye bandari bubu ili kudhibiti vitendo hivyo.

# Mmoja walioungua meli ya mafuta afariki dunia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MFANYAKAZI mmoja kati ya watatu wa meli ya mafuta ya Mt. Ukombozi walioungua wakati wakisafisha kisima cha mafuta, amefariki dunia wakati akiendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Aliyefariki ni Ali Juma Ame ambaye alikutwa na mauti hayo juzi katika hospitali hiyo, huku majeruhi wenzake wawili wakiendelea kupata matibabu.

Wafanyakazi hao waliungua baada ya meli hiyo kushusha mafuta katika Bandari ya Wesha Wilaya ya Chakechake Pemba Oktoba 10, mwaka huu majira ya asubuhi, wakati wakiwa katika majukumu yao ya kazi.

Daktari wa Upasuaji wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Sali Ali Said, alisema hali za majeruhi hao bado si nzuri kutokana na kuungua vibaya sehemu kubwa ya miili yao.

"Majeruhi wameungua vibaya hasa tumboni, uso na miguu na tunaendelea kuwapatia matibabu," alisema.

Alisema kwa hatua ya mwanzo majeruhi hao walifikishwa katika chumba cha upasuaji kwa ajili ya kufanyiwa upasuaji mdogo ikiwamo kuondosha ngozi zilizoungua.

Alisema huenda majeruhi hao wakasafirishwa kupelekwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) kutokana na Hospitali ya Mnazi Mmoja kukosa kitengo cha wagonjwa watu wazima walioungua moto.

Msemaji wa hospitali hiyo, Hassan Makame, alisema majeruhi hao waliwasili saa 7:30 za mchana Oktoba 10 wakitokea Pemba na kupokelewa kitengo cha dharura.

Alisema mpaka sasa majeruhi wawili waliobaki wapo katika chumba cha uangalizi maalum (ICU) wakiendelea kupatiwa matibabu, ingawa hali zao haziridhishi na kwamba mwili wa aliyefariki dunia ulishakabidhiwa kwa familia yake kwa ajili ya mazishi.




Mwandikishaji wapigakura wa kituo cha Mtaa wa Machimbo Kata ya Yombo Vituka, Mwajabu Omary Mndolwa, akimwandikisha Crispo Donald mmoja wa wananchi wa kata hiyo, jijini Dar es Salaam, jana, baada ya uhamasishaji uliofanywa na viongozi wa eneo hilo. Wengine ni Sijali Ramadhani ni wakala wa CCM (kulia), Lusajo Mwakatumbula wakala wa Chadema. **PICHA NA MPIGA PICHA WETU.**

# Sababu wanawake vijijini kukosa hati za ardhi yatajwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UKOSEFU wa taaluma ya umiliki wa ardhi umechangia wananchi wengi wa vijijini, hususani wanawake kukosa kumiliki hati za matumizi ya rasilimali ya ardhi.

Hayo yalielezwa na Ofisa Mwandamizi kutoka Kamisheni ya Ardhi, Haji Mrisho, alipokuwa akitoa ufafanuzi juu ya umuhimu wa kumiliki rasilimali hiyo kwa wananchi wa Kijiji cha Matemwe katika Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema hali hiyo huchangiwa na wananchi wengi, kuvamia maeneo bila ya kufuata taratibu na kusababisha kutokea migogoro mingi ya ardhi inayosababisha kupoteza mali na maisha yao.

Alisema haiwezekani wananchi kumiliki rasilimali hiyo kwa maneno matupu, bila ya kufika serikalini na kufuata taratibu za kisheria juu ya umiliki huo.

Naye Bahati Issa kutoka Mtandao wa Ardhi Wilaya ya Kati Unguja, alisema ardhi ni rasilimali muhimu kwa ajili ya maendeleo.

Kutokana na umuhimu huo, aliwataka wanawake wenzake kulipa umuhimu suala hilo ili kuepuka kudhulumiwa na waweze kupata haki zao.

Baadhi ya wananchi wa kijiji hicho walikishukuru Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) kwa upande wa Zanzibar, kwa kwenda kuwafumbua macho kwa kuwapatia elimu hiyo.

Walieleza kuwa wana maeneo ya ardhi wanayomiliki, lakini hawana hati za utambuzi wa maeneo hayo, hivyo elimu waliyopatiwa wameifurahia na watafanya juhudi ya kuhakikisha wanakuwa na hati ya utambuzi wa ardhi.

Baada ya kuwapo kwa malalamiko mingi ya migogoro ya ardhi hasa kwa wanawake, TAMWA-Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Foundation for Civil Society, imekua ikitoa elimu ya umuhimu wa umiliki wa ardhi ili kupunguza migogoro hiyo.

# Wenye maumivu ya shingo, mgongo kuchunguzwa Dar

**Na Mwandishi Wetu**

WATAALAMU bingwa wa maradhi ya maumivu ya mgongo, shingo na uti wa mgongo kutoka India wanatarajia kuwafanyia uchunguzi Watanzania wenye matatizo ya aina hiyo na kuwapa matibabu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Hospitali ya Regency, uchunguzi huo unatarajiwa kufanyika katika Hospitali ya Regency mwezi huu.

Ilisema kwenye taarifa hiyo kuwa jitihada hizo ni kutaka kupunguza rufani za wagonjwa wanaokwenda nje ya nchi kwa matibabu hali itakayosaidia kuwaondolea gharama wagonjwa kwa kupata matibabu ya kibingwa hapahapa nchini.

Ilisema wataalamu hao watafanya uchunguzi wa matatizo mbalimbali ya mgongo kama maumivu ya shingo, maumivu ya uti wa mgongo na mengine yanayohitaji utaalamu wa hali ya juu kama upasuaji.

"Uchunguzi huu utafanyika tarehe 25 na 26 wiki hii hapa Regency na hii ni fursa nzuri kwa Watanzania kuja kuchunguzwa na kupatiwa matibabu ya kibingwa badala ya kutumia gharama kubwa kwenda India," ilisema taarifa hiyo.

"Hii ni fursa ya pekee kwa Watanzania wenye matatizo ya maumivu ya shingo, mgongo na uti wa mgongo kuja kuonana na wataalamu kwa ajili ya kupata tiba ambayo wangepaswa kusafiri kwenda India," ilisema taarifa hiyo na kuwa utaanza Oktoba 25 hadi 26.

# UNFPA, wadau waanzisha vita mila potofu kuelekea 2030

**Na Yasmine Protace**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) ofisi ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwamo serikali, wamejipanga kutokomeza matukio ya mila potofu na unyanyasaji wa kijinsia kwa watoto wa kike, kuelekea mwaka 2030.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam na Warren Bright, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa UNFPA nchini katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani, ambayo huadhimishwa duniani Oktoba na mwaka huu kauli ni 'nguvu ya binti haizuiliki'.

"Changamoto kubwa ambayo tunaangalia inayomkabili mtoto wa kike ni ndoa za utotoni, ukeketaji na kubwa zaidi kwenye makuzi tunaangalia masuala ya hedhi salama," alisema.

Aliongeza kuwa kuelekea mwaka 2030, katika malengo ya dunia kuna sehemu kubwa ambayo watahakikisha wanatokomeza mila potofu na unyanyasaji wa kijinsia kwa watoto wa kike.

Aliongeza kuwa, ukatili wa kijinsia kwa watoto wa kike ni matukio ambayo yanasababisha kuwa na chimbuko la ukeketaji na ndoa za utotoni.

Alisema wanaungana na wadau mbalimbali ikiwamo serikali kwa kusherehekea mafanikio kwa sababu elimu ya afya ya uzazi kwa mabinti wengi imeonyesha kuzaa matunda baada ya kujitambua kuhusu afya ya uzazi.

Akizungumzia suala la ukeketaji, alisema wamepiga hatua kubwa kwa kuhakikisha wanafanya kazi kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda ambapo wameingia katika mkakati ambapo maeneo ya mipakani wamekuwa wakitoa elimu ambayo imesaidia watu kutoka nchini kwenda Kenya na Uganda kwa ajili ya kukeketwa, sasa hawaendi.

"Kulikuwa na baadhi ya watu walitumia maeneo ya mipakani Kenya na Uganda kwa ajili ya kuwakeketa watu, lakini baada ya elimu kutolewa sasa matukio hayo hayapo," alisema.

Aliongeza kuwa wamekuwa wakifanya kazi kwa pamoja na kushirikiana na ngariba na wazee wa kimira ambapo ushirikiano huo umezaa matunda, na hali hiyo imesaidia hata wale waliokuwa wakikeketa mabinti waliweza kuzitupa nyembe.



Mafundi wakiutoa mfuniko wa mtaro eneo la Gerezani jijini Dar es Salaam ili kuondoa taka zilizoziba na kusababisha kujaa maji ya mvua barabarani juzi. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Wasioona, wenye saratani wasaidiwa

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Maendeleo TIB imeunga mkono jitihada za serikali katika kusaidia masuala ya afya kwa kuwasaidia fimbo nyeupe 86 Chama cha Watu Wasioona - Wilaya ya Temeke.

Pia imetoa Sh. 2,500,000 kama sehemu ya mchango wa ununuzi wa matiti bandia 2,500 kwa waathirika wa saratani ya matiti kwa Taasisi ya Kuwasaidia Waathirika wa Saratani - TCS HOPE.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo TIB, Charles Singili, alisema TIB ni Taasisi ya Maendeleo inachukulia ustawi wa wahitaji wenye changamoto za kiafya kama mojawapo ya kichocheo muhimu cha maendeleo.

Aliongeza kuwa kwa kutambua umuhimu wa sekta ya afya katika kuleta maendeleo ya nchi, benki hiyo itaendelea kutoa michango hiyo ili kuwasaidia wahitaji wenye mahitaji maalum ya kiafya pamoja na kuunga mkono juhudi za serikali katika masuala ya afya.

Alisema kuwa kutambua kazi nzuri inayofanywa na serikali, katika kukuza maendeleo ya sekta ya afya, elimu, utengenezaji ajira na ujasiriamali benki hiyo imejipanga kuendelea kusaidia jitihada hizo kwa kuwekeza katika miradi ya kimkakati itayosaidia kuongeza kasi ya maendeleo nchini.

"Lengo letu ni kusaidia jitihada za serikali ili kuongeza kasi ya kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo hususani katika kusaidia nchi yetu kufikia uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025," alisema.

Akizungumzia msaada walioutoa, Singili alisema fimbo zilizotolewa ni nyenzo na visaidizi muhimu kwa wasioona ambavyo zinamsaidia mtu asiyeona aweze kufanya safari zake popote anapotaka kwenda bila kuathiriwa na watumiaji wengine wa barabara.

"Napenda kuiomba jamii na hasa watumiaji wote wa miundombinu ya barabara watembea kwa miguu, madereva wa magari, pikipiki (daladala/bodaboda) watumiaji wa vyombo vyote vya moto kuheshimu fimbo nyeupe na kuwasaidia wasioona wawapo barabarani," Singili alisema.

Katibu wa Chama cha Watu Wasioona - Wilaya ya Temeke, Protase Mutakyanga, alisema kuwa mchango uliotolewa na benki hiyo, utasaidia wanachama wake kuweza kuendelea kujishughulisha na masuala ya kujitafutia kipato.

Katibu wa TCS Hope, Luca Mabena, alishukuru kwa mchango huo ambao alisema utasaidia kurejesha furaha kwa kina mama walioathirika na saratani ya matiti.

HABARI KIMATAIFA

# Tunisia wapiga kura kumpata rais mpya

**TUNIS, Tunisia**

WANANCHI zaidi ya milioni saba wa Tunisia jana, walijitokeza kwa wingi katika vituo vya kupiga kura kwa lengo la kumchagua kiongozi mpya atakayeliongoza taifa hilo kwa miaka mingine.

Viongozi wanaochuana kwa karibu kuwania nafasi hiyo ni Profesa wa Sheria, Kais Saied na mmiliki wa vyombo vya habari, Nabil Karoui.

Wanasiasa hao wapya walifanikiwa kuwaondosha wagombea urais katika duru ya kwanza, hatua iliyodhihirisha uchungu wa wapigakura na kutofaulu kwa maofisa kukabiliana na mkwamo wa uchumi, ukosefu mkubwa wa ajira na huduma duni za umma.

Vituo vya kupigia kura vilifunguliwa majira ya saa 2:00 asubuhi kwa ajili ya duru ya pili na ya mwisho ya uchaguzi huo, ambapo saa 12 za kupiga kura zitaamua kiongozi wa pili wa nchi hiyo ya Afrika Kaskazini.

Kampeni ya uchaguzi wa urais nchini humo zilianza Ijumaa

Kais Saied, ambaye alipata asilimia 18.4 ya kura katika duru ya kwanza, anapambana na mfanyabiashara Nabil Karoui, aliyepata asilimia 15.58.

Mapema wiki hii mahakama ilimwachilia huru Karoui, ambaye alikuwa kizuizini tangu Agosti 23 kwa madai ya utakatishaji fedha na ukwepaji kodi.

Wananchi wa Tunisia walitoa maoni yao kuhusu uchaguzi huo na kuweka wazi matatizo yanayoikabili nchi yao kwa sasa.

Hali ya uchumi Tunisia iko mashakani, idara mbalimbali za umma hazifanyi kazi vilivyo, kunaripotiwa ukosefu wa ajira, na pia mfumko wa bei unaendelea kushuhudiwa nchini humo, wananchi wengi wa Tunisi wanataka hali zao za maisha kuboreshwa.

"Nilifanya kazi kwa miaka 35 katika Wizara ya Vijana, ninajitahidi kufanya kazi katika mgahawa huu ili kupata ruzuku. Nina watoto wawili wa kiume; mmoja yuko nje ya nchi, na anafanya kazi katika Shirika la Mpango wa Chakula Duniani, WFP; mwingine hana kazi tangu mwaka 2014. Ana nia ya kuondoka nchi hii kwa sababu hapa hakuna matarajio ya vijana," alisema Adel Tounes, mtumishi wa umma aliyestaafu.

Katika duru ya kwanza ya uchaguzi wa urais, asilimia tisa tu ya vijana wenye umri wa miaka 18 hadi 25 ndio walipiga kura.

Kwa mujibu wa mwanasaikolojia, Omar Zafouri kutoka Chuo Kikuu cha Sfax, alieleza kuwa hali hiyo inaweza kuwa moja ya sababu ya masuala ya kielimu.

"Kadri umri unavyoongezeka, kiwango cha ushiriki kinaongezeka; asilimia tisa kwa vijana wadogo, asilimia 33 kwa watu wazima, na asilimia 57 kwa watu walio na umri wa miaka zaidi ya 50," alisema Prof. Zafouri.

**RFI**

# Papa amtangaza Kardinari Newman mtakatifu mpya

**ROME, Italy**

PAPA Francis jana alimtangaza Kardinari John Henry Newman kuwa mtakatifu.

Papa Francis alimtanga katika maadhimisho ya misa aliyoiongoza jana mjini Rome, Italia.

Misa hiyo iliyokuwa ya wazi ilihudhuriwa na maelfu ya watu waliofika katika ibada hiyo.

Kardinari Newman, ambaye alifariki mjini Birmingham mwaka 1890, anakuwa ni Mwingereza wa kwanza kutangazwa kuwa mtakatifu kwa kipindi cha takribani miaka 50.

Miongoni mwa viongozi waliohudhuria misa hiyo ambayo ilikuwa inawatambua wanawake wengine wanne kuwa watakatifu ni mwana mfalme wa Wales

Mama Mariam Thresia kutoka India, Marguerite Bays kutoka Uswizi, Mama Giuseppina Vannini kutoka Italia na sista aliyezaliwa Brazili Dulce Lopes Pontes walikuwa wanatambuliwa pia kuwa watakatifu katika misa hiyo.

Maelfu ya Waingereza walisafiri mpaka mjini Rome ili kusherehekea utambulisho huo.

Katibu wa marafiki wa Newman kutoka mji wa Birmingham, Carol Parkinson, alisema kuwa kutangazwa kwa mtakatifu huyo ni kwa kipekee na imekuwa siku ya hisia kubwa kwao.

"Uadilifu wake, urafiki wake, uaminifu pamoja na bidii aliyoweka katika kazi yake ni mfano mzuri wa kuigwa na kila mtu," alisema Parkinson.

Kardinali Newman alizaliwa mjini London Uingereza mwaka 1801, alisoma Chuo cha Trinity College na Oxford.

Alikuwa anatarajiwa kuwa padri wa Kianglikana lakini alibadili dhehebu na kuwa Mkatoliki mwaka 1845.

Newman amesifika kwa miujiza miwili, muujiza wa kwanza ni kumponya mgonjwa wa uti wa mgongo, na kumponya mwanamke aliyekuwa aachi kutokwa damu. ***BBC***



Wanawake wakikimbia baada ya roketi kurushwa kwenye mji wa Akcakale. **PICHA: REUTERS**

# Meli ya mafuta Iran yashambuliwa, yalipuka

**TEHRAN, Iran**

MELI ya mafuta ya Iran inadaiwa kushambuliwa karibia na Pwani ya Saudi Arabia, hali iliyosababisha mlipuko uliosababisha moto mkubwa kutokea.

Vyombo vya habari vya Iran vimeripoti kuwa meli hiyo inayomilikiwa na Shirika la Kitaifa la Mafuta la Iran (NIOC) ilikuwa umbali wa maili 60 sawa na kilometa 97 kutoka Bandari ya Saudi ya Jeddah.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Iran inadai kuwa meli hiyo ilishambuliwa mara mbili.

Taarifa iliyotolewa na Msemaji wa Wizara hiyo, Abbas Mousavi Said ilieleza kuwa katika miezi ya hivi karibuni visa na hujuma vimekuwa vikitekelezwa dhidi ya meli za mafuta za Iran katika bahari nyekundu, kwamba uchunguzi bado unaendelea kutokana na tukio hilo.

Mwishoni mwa wiki vyanzo vya habari ambavyo havikuthibitishwa viliarifu vyombo vya Iran kwamba meli hiyo ililipuliwa kwa makombora ambayo huenda yalikuwa yanatoka Saudi Arabia.

Lakini NIOC baadaye ilikanusha madai hayo na kueleza kuwa milipuko miwili tofauti ilitokea katika meli hiyo ambayo huenda imesababishwa na makombora.

Hata hivyo, milipuko hiyo haijathibitishwa na taarifa kuhusu meli haijawekwa wazi.

Televisheni ya kitaifa ya Iran awali iliripoti kuwa meli hiyo imetambuliwa kama Sinopa, lakini NIOC baadaye ilisema inaitwa Sabiti.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa hifadhi mbili za mafuta zimeripotiwa kuharibiwa, hali iliyosababisha mafuta kumwagika katika bahari nyekundu lakini hakuna mtu aliyejeruhiwa.

Picha zinazodaiwa kupigwa siku ya Ijumaa katika meli hiyo zilionyeshwa katika Televisheni ya Taifa ya Iran lakini hazikuonyesha uharibifu wowote.

Chanzo kutoka katika kampuni ya Windward inayojishughulisha na uchambuzi wa masuala ya baharini iliiambia Shirika la Utangazaji la BBC kuwa ni jambo la kawaida kwa meli za mafuta za Iran kuzima AIS ili isionekane - mara kwa mara kuepuka vikwazo vya kimataifa na unyanyasaji kutoka kwa Saudi Arabia.

Kutokana na sababu za kiusalama meli zote huzima kifaa cha AIS zinapokaribia mfereji wa Suez.

Tukio hilo linajiri wakati kumekuwa na hali ya taharuki kati ya Iran na Saudi Arabia katika siku ya hivi karibuni.

Mwezi uliopita ndege 18 zisizokua na rubani na makombora saba ya meli zilishambulia visima vya mafuta na kituo cha kusafisha mafuta nchini Saudi Arabia, shambulio ambalo Saudia ililaumu Iran.

Maofisa wa Marekani walisema Iran ilihusika katika mashambulio dhidi ya meli mbili za mafuta katika eneo la Ghuba mwezi Juni na Julai, na pia kushambulia meli zingine nne za mafuta mwezi Mei.

Lakini, Iran ilipinga madai ya kuhusika na matukio hayo.

***BBC***

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA LINAUZW**A, Hekari 25@Tshs 800,000/= ziko Miono Kijiji cha Mkange Wilaya ya Chalinze (kuelekea Sadani Game Reserve) mwendo dakika 40 toka barabara kuu iendayo Tanga. Wasiliana na 0713 604049 / 0784 604049.


## *NIPASHE NI JIBU LAKO*

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**RAYMOND MUSA URASSA** MKAZI WA MAJENGO SHINYANGA MJINI ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YAKE YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 919 AVA** AMBAYO ILIPOTEA MWAKA 2018 MAENEO YA MAJENGO MAPYA KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA RAYMOND MUSA URASSA KWA SIMU NAMBA **0715048014**

**SHY/RB/2019,** KUMBUKUMBU YA MALIPO NAMBA **9910810124187.**

115460202

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI.

**GEORGE CHABBY HAULE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA SURF** yenye namba za usajili **T366BKL** Chassis namba **RZN1859011609** Engine no **3RZ1542498** .Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:

**DSM/PHQ/RB377215/2019**

115460202

SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI YA MWAKA 1999

(SURA YA 113)

KUHAMISHA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI

MMILIKI ALIYEANDIKISHWA: SALIMA SAIDI

KWENDA KWA: RITHA MAHIMBO

ARDHI: KIWANJA NA. 524 KITALU 'B' ENEO LA KIBONDEMAJI-MBAGALA

MANISPAA YA TEMEKE JIJINI

DAR ES SALAAM.

Taarifa inatolewa kwamba AFISA ARDHI MTEULE anakusudia kuhamisha BARUA YA TOLEO TAJWA YA KUMILIKI ARDHI kwenda kwa RITHA MAHIMBO aliyewasilisha barua ya toleo pamoja na mkataba wa manunuzi kwamba ameuziwa kiwanja hicho, ikiwa kwa jina la SALIMA SAIDI. Ninakusudia kutoa HATI MILIKI iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa siku 30 tangu tarehe ya taarifa hii ilipotangazwa katika gazeti.

115460102


***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0767 223311***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO



# MESSI

## SASA KUFUNGWA MAISHA HAPO BARCA

**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona wapo kwenye mpango wa kukamilisha kumpa, Lionel Messi mkataba wa maisha ili amalize miaka yake yote ya maisha ya soka pale kwenye dimba la Nou Camp.

Mkataba wa sasa wa Messi unafika mwisho Juni 2021, hiyo ina maana kwamba itakapofika mwisho mwa msimu huu ataingia kwenye mwaka wa mwisho wa kwenda kuwa mchezaji huru kama hakutakuwa na dili jipya litakalosainiwa.

Kulikuwa na wasiwasi juu ya Messi kuondoka kwenye kikosi hicho kwa sasa, lakini mwenyewe hivi karibuni alifichua kwamba nanye alikuwa na hofu kwamba huenda asingepewa dili jipya la kubaki kuitumikia timu hiyo iliyomsajili tangu akiwa mtoto mdogo.

Kwa mujibu wa Cadena Ser, Barcelona mpango wao ni kumpa mkataba mpya nyota huyo ili abaki kwenye timu yao kwa maisha yote.

Na kwa mujibu wa taarifa ya miamba hiyo ya Hispania inataka kumpa Messi mkataba wa maisha ili abaki kwenye timu yao pengine kwa miaka mingine 10 kuanzia sasa.

Novemba 2017, Messi alisaini makubali ya kubaki kwenye timu hiyo kwa dili lenye thamani ya euro milioni 70, huku kiwango hicho kikiongezeka na kufikia euro milioni 100 kutokana na malipo ya haki za matangazo pamoja na bonasi ya usajili.

## RONALDO VITANI LEO AKITAFUTA LA 700

**LISBON, Ureno**

CRISTIANO Ronaldo atakuwa na nafasi ya kufikisha mabao 700 wakati Ureno ikiivaa Ukraine leo endapo atacheka na nyavu mara moja tu, kufuatia kutupia wavuni wakati wakiifunga Luxembourg mabao 3-0 kwenye michuano ya kufuzu fainali za euro 2020.


Bao la mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 34, aliofunga kwenye dakika ya 65 lilikuwa la 699 kufunga katika mechi 973 alizocheza na klabu na timu ya taifa.

Staa wa Manchester City, Bernardo Silva, aliifungia bao la kuongoza Ureno katika kipindi cha kwanza kabla ya Ronaldo kufunga la kwake na Goncalo Guedes kuhitimisha bao la tatu dakika moja kabla ya filimbi ya mwisho.

Ushindi huo umewafanya Ureno kupunguza pengo la pointi kwenye Kundi B dhidi ya vinara Ukraine, ambao waliwapiga Lithuania 2-0 na pengo sasa kuwa pointi tano huku wakiwa na mchezo mmoja mkononi, utakaopigwa leo Jumatatu.

Kwenye usiku wa rekodi, Andorra wameandikisha ushindi wao wa kwanza mchezo wa kufuzu wa michuano hiyo ya Ulaya.

Katika mechi hiyo, Andorra ilicheza mara 56 kwenye mechi za kufuzu na kupoteza zote. Lakini, sasa walipata ushindi wao wa kwanza kwa kuwafunga Moldova 1-0 kwenye Kundi H. Kwingineko, kiungo N'Golo Kante alizua hofu baada ya kupata majeraha ya misuli wakati akipasha misuli moto kwenye mchezo wa Ufaransa dhidi ya Iceland, ambapo Les Bleus walishinda 1-0 shukrani kwa bao la mkwaju wa penalti la Olivier Giroud. Ufaransa sasa wamefikisha pointi 18 sawa na Uturuki kwenye Kundi H.



## RODRI AIKATIA TAMAA MAN CITY

**MANCHESTER, England**

RODRI anaamini kwamba, Manchester City si tena timu bora kwenye Ligi Kuu England na kusisitiza kwamba taji hilo kwa sasa linashikiliwa na Liverpool.

Liverpool ya kocha Jurgen Klopp ilishuhudia msimu uliopita ikipigwa kikumbo na Man City kwenye ubingwa wa Ligi Kuu England kwa tofauti ya pointi moja tu, lakini msimu huu wamekuwa kwenye moto ambapo kwa sasa wameweka pengo la pointi nane kileleni baada ya mechi nane kupigwa.

Sambamba na hilo, Liverpool ndiyo timu pekee kwenye Ligi Kuu England msimu huu ambayo imeshinda mechi zote, wakati Man City ya kocha Pep Guardiola imeanza kampeni ya kutetea taji lao hilo kwa kusuasua, wakiwa wamechapwa mara mbili katika mechi nane.

Na sasa kiungo mpya wa wababe hao wa Etihad, Rodri anaamini kwamba Liverpool ndio timu bora kwa sasa England na Ulaya.

Rodri aliulizwa ni timu gani atapenda kuifunga, Liverpool au mahasimu wao Manchester United, alijibu: "Sifahamu."

"Sifahamu mambo ya kwenye jiji hili, sifahamu watu wanavyojisikia. Lakini, ukisema timu tamu ya kuifunga kwa sasa ni Liverpool. Ni mabingwa wa Ulaya kila mtu anataka awafunge, si sisi tu. Ukweli wao ni timu bora, wameboresha kila kitu, wana timu nzuri ukweli ni timu bora England na Ulaya."

Rodri aliwasili Man City akitokea Atletico Madrid kwa ada ya Pauni milioni 62.8, ada iliyoweka rekodi kwenye klabu hiyo ya Etihad.



## HABARI MICHEZO



# MESSI, AGUERO KURUDI ARGENTINA NOVEMBA

**BUENOS AIRES, Argentina**

NAHODHA wa Argentina, Lionel Messi, atarudi kwenye timu ya taifa Novemba baada ya kufungiwa, amesisitiza kocha wa timu hiyo ya taifa, Lionel Scaloni.

Messi alifungiwa mechi tatu za kimataifa Agosti kwa kuwashutumu viongozi wa Shirikisho la Soka la Amerika Kusini (CONMEBOL), kwa rushwa wakati wa michuano ya Copa America.

Baada ya kutolewa nje kwa kadi nyekundu ya utata katika mchezo wa kusaka nafasi ya tatu ya ushindi wa Argentina dhidi ya Chile Julai, Messi alikataa kwenda kuchukua medali yake na mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or, baadaye alieleza kwamba hakutaka kuwa sehemu ya rushwa.

Messi pia aliwabwatukia waamuzi wa mchezo huo baada ya Argentina kutolewa kwenye nusu fainali na Brazil, kwamba walikuwa wamekipanga kikosi hicho cha kocha, Tite kutwaa kombe hilo.

Messi amekosa kuichezea Argentina mechi ya kirafiki dhidi ya Chile, Mexico na Ujerumani.

Alipoulizwa kuhusu Messi, Scaloni aliwaambia waandishi wa habari: "Messi hayupo hapa kwa sababu amefungiwa.

"Sergio Aguero hayupo hapa kwa sababu ni majeruhi na hajawa kwenye mazoezi kwa sababu bado hayupo fiti kwa asilimia 100.

"Kwa uhakika wote watakuwa na timu mwezi ujao."

# Southgate ageukia mbinu Kombe la Dunia

**LONDON, England**

GARETH Southgate atarudi kwenye mfumo wake wa kuchezesha mabeki watatu kwenye ulinzi kama England ilivyocheza kwenye michuano ya Kombe la Dunia baada ya kufungwa na Jamhuri ya Czech.

England ilifungwa mabao 2-1 na kuwafanya wasitangulie kufuzu kwa michuano ya Euro 2020.

Kiwango duni kilichoonyeshwa pale Prague kimemlazimu kocha, Southgate kufikiria mbinu nyingine na sasa ataamua kurudi kwenye mfumo alioutumia katika michuano ya Kombe la Dunia nchini Urusi.

Harry Maguire, John Stones na Kyle Walker, ambao kwa sasa walitemwa kwenye kikosi, walitengeneza safu ya walinzi watatu na kufanikiwa kufika nusu fainali ya michuano hiyo.

"Ni kitu ambacho natakiwa kukifikiria upya na sidhani kama tutashindwa kufuzu," alisema Southgate.

"Nafikiri tupo kwenye wakati mgumu hasa katika suala la wachezaji ambao wanacheza mara kwa mara timu ya taifa na pia kwenye klabu zao.

"Na hiyo ni moja ya sababu kwa nini hatukuwachezesha walinzi watatu kwenye mchezo dhidi ya Czech."



# Ozil kupelekwa kwa mkopo Fenerbahce

**LONDON, England**

ARSENAL imeripotiwa kwamba, ipo katika mazungumzo na Klabu ya Fenerbahce ya Uturuki kwa ajili ya kuipata saini ya nyota wake, Mjerumani Mesut Ozil.

Uhamisho wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, utakuwa ni wa mkopo huku Arsenal ikiendelea kulipa sehemu ya mshahara wake mkubwa wa pauni 350,000 kwa wiki.

Ozil atatimiza umri wa miaka 31, wiki ijayo na anajua atalazimika kwenda kwingine kwa ajili ya kupata nafasi ya kudumu katika dirisha la Januari.

**Emery amemwondoa Ozil katika mipango yake na amependelea zaidi kuwa panga makinda klabuni hapo huku ikiaminika kwamba anataka kuachana na staa huyo katika dirisha la Januari.**

Kwa ujumla, Ozil amecheza mchezo mmoja tu wa Ligi Kuu England katika msimu huu, akiingia dhidi ya Watford ambao uliisha kwa sare ya mabao 2-2.

Kocha Emery amekuwa akiwapa nafasi zaidi Dani Ceballos na kinda Joe Willock kufanya majukumu ya kucheza kwenye nafasi ya namba 10.

Tangu kutua kwa Emery hapo Arsenal, Ozil amekuwa hana nafasi kwa kocha huyo na mara kadhaa amekuwa akitamka kwamba, hamhitaji na hivyo, amekuwa akipigania kumwondoa kwenye kikosi chake.

Ozil ambaye alisajiliwa kutoka Real Madrid ya Hispania alikuwa na wakati mzuri zaidi alipotua hapo chini ya kocha Arsene Wenger, lakini sasa siku zake zinaonekana kufikia mwisho kwa 'Washika Bunduki' hao wa London.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BECKHAM AMPONGEZA RAMOS REKODI HISPANIA

Lazima ujisikie fahari sana, familia yako lazima ijisikie fahari sana, ni wakati mzuri sana, kumpiku Iker...

**MADRID, Hispania**

DAVID Beckham amempongeza Sergio Ramos baada ya kuvunja rekodi ya kucheza mechi nyingi timu ya Taifa ya Hispania iliyokuwa ikishikiliwa na kipa Iker Casillas.

Ramos, alitimiza mechi 168 wakati wakitoka sare bao 1-1 dhidi ya Norway kwenye mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 juzi, Jumamosi.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 33, ambaye alianza kuichezea timu hiyo kwa mara ya kwanza mwaka 2005, mwezi uliopita aliifikia rekodi hiyo ya Casillas kabla ya juzi kuivunja rasmi, na mmoja wa wachezaji wa kizazi cha dhadhabu waliobaki kikosini hapo ambao walitwaa Kombe la Dunia na lile la Ulaya.

Hivyo, mchezaji mwenza wa zamani katika kikosi cha Real Madrid, Beckham akampongeza Ramos kupitia ukurasa wake wa Instagram akimtumia ujumbe kwa njia ya video, akisema: "Rafiki yangu, 'mi amigo'.

"Huu ni wakati mzuri sana kwako. Ninataka kutuma ujumbe tu kwa sababu umecheza mechi 168 kwa nchi yako.

"Lazima ujisikie fahari sana. Familia yako lazima ijisikie fahari sana. Ni wakati mzuri sana, kumpiku Iker.

"Hivyo, ni mwenye furaha sana kwako na familia yako. Hongera rafiki yangu, busu kwako. Ufurahie usiku huu. Mapenzi makubwa rafiki yangu na hongera."

Bao la Saul Niguez la kipindi cha kwanza lilisawazishwa na Josh King kwa penalti ya dakika za majeruhi na kuzima rekodi ya Hispania ya asilimia 100 ya kushinda mechi zote za Kundi F kwenye kinyang'anyiro hicho.

Ikitoka sare na Sweden kesho Jumanne itaifanya Hispania kufuzu kwa michuano hiyo ya Ulaya.

"Yote hayo ni binafsi na ni mambo madogo," alisema Ramos baada ya mchezo huo.

"Ningekuwa na furaha zaidi kucheza mechi yangu ya 168 kwa kupata ushindi. Haikuwa shida. Lakini rekodi hii ni kubwa na tuzo nzuri kwangu baada ya miaka mingi ya kuichezea timu yangu ya taifa.

"Nijisikia furaha kila wakati kwa kile nilichofanya nikiwa na jezi hii. Hilo halitabadilika na kuendelea kufanya hivyo kwa miaka mingi."

Hispania ilionekana inaelekea kushinda mchezo wake wa saba mfululizo kwenye kufuzu hadi pale golikipa wa Chelsea, Kepa Arrizabalaga alipomdondosha, Omar Elabdellaoui ndani ya 18.

Mchezaji wa Bournemouth, King alifunga penalti dakika ya 94 na kuwaacha Norway wakiwa nafasi ya nne kwenye kundi hilo la F.

Ramos, ambaye ameipiku rekodi ya mchezaji wa Latvia, Vitalijs Astafjevs kwa kuwa mchezaji aliyeichezea nchi yake mechi nyingi zaidi Ulaya, sasa amebakisha mechi nane kuifikia rekodi ya Gianluigi Buffon aliyeichezea Italia mechi 176.

Beki huyo ana safari ya kwenda kuvunja rekodi zaidi, ingawa mshambuliaji wa zamani wa Misri, Ahmed Hassan ndiye aliyeichezea nchi yake mechi nyingi zaidi (mechi 184) kati ya mwaka 1995 na 2012.

## KWA UFUPI

**BAYERN, REAL KWA ERIKSEN**

Bayern Munich inaweza kutoa upinzani kwa Real Madrid katika mbio za kumnasa kiungo wa Tottenham, Christian Eriksen na kwenda kumfuata Mdenmark huyo mwenye umri wa miaka 27, katika dirisha la usajili la Januari. ***(Sport1, via Mirror)***

**GERRARD KUMTOA DEFOE**

KOCHA wa Rangers, Steven Gerrard amefunguka kuwa mshambuliaji wa zamani wa England, Jermain Defoe, 37, anayeichezea klabu hiyo kwa mkopo atapewa majukumu ya ukocha kwa miamba hiyo Ibrox msimu ujao. ***(Daily Record)***

**FERNANDINHO MWAKA CITY**

KIUNGO wa Manchester City, Mbrazil Fernandinho, 34, ambaye atamaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu huu, yupo mbio kupewa mwingine mpya wa mwaka mmoja. ***(Sun)***

**PARKINSON ANUKIA SUNDERLAND**

KOCHA wa zamani wa Bolton, Phil Parkinson yupo katika nafasi nzuri zaidi ya kuwa kocha mpya wa Sunderland. ***(Star)***

**SOLSKJAER AANZA KUTAPATAPA**

Ole Gunnar Solskjaer anaitaka Manchester United kutumia huduma ya washauri wa Hispania kuendesha suala la ajira katika klabu hiyo. ***(Mail)***

**LUKAKU, SANCHEZ WAKUMBUKWA**

Manchester United inatarajiwa kuwa na kiasi cha pauni milioni 300 za kutumia sokoni katika majira ya misimu miwili ijayo lakini nahodha wao wa zamani, Bryan Robson anasema ilikuwa ni kosa kubwa kupoteza majina makubwa akiwamo mshambuliaji Mbelgiji Romelu Lukaku, 26, na straika Mchile Alexis Sanchez, 30, bila kuziba mapengo yao. ***(Star)***

**FABIANSKI NJE MIEZI MI3**

KIPA wa West Ham, Mpoland Lukasz Fabianski, 34, anatarajiwa kuwa nje ya kikosi kwa miezi mitatu baada ya kufanyiwa upasuaji wa paja. (London Evening Standard)

**WOLVES YAMTAKA LUYINDAMA**

Wolves imekuwa ikihusishwa na kumsajili beki wa Galatasaray, Mcongo Christian Luyindama, 25, ambaye zamani alikuwa akiwindwa na Aston Villa. ***(Birmingham Mail)***

**NEWCASTLE KUMBEBA BRUCE**

Newcastle inapanga kutoa sapoti kwa kocha Steve Bruce katika dirisha la usajili la Januari, wakati suala la usajili tayari tayari likiwa njiani hapo St James' Park. ***(Newcastle Chronicle)***

**ERIKSSON ATESEKA NA ENGLAND**

KOCHA wa zamani wa England, Sven-Goran Eriksson amesema bado anasumbuliwa na namna sehemu ya vyombo vya habari vilivyohusika katika kufukuzwa kwake kwenye timu ya hiyo ya taifa. ***(Times)***

**VAN DER SAR AITAMANI UNITED**

KIPA wa zamani wa Manchester United, Edwin van der Sar, ambaye kwa sasa ni mkurugenzi mkuu wa Ajax, amefunguka kwamba angependa siku moja kurudi Old Trafford - kama atapata nafasi kama anayoitumikia kwa sasa. (Mirror)

**NEWCASTLE YAMWINDA MANNING**

Newcastle inamfuatilia kiungo wa QPR na Jamhuri ya Ireland, Ryan Manning, 23. ***(Football Insider)***



## HABARI MICHEZO

# KOCHA WA JAMHURI: UMASKINI UNATUTESA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA msaidizi wa timu ya Jamhuri inayoshiriki Ligi Kuu ya Zanzibar, Mfaume Shabaani amesema kufanya vibaya kwa timu yake kunatokana na umaskini wa kifedha unaoikabili timu hiyo ya kisiwani Pemba.

Akizungumza na gazeti hili kocha huyo alisema timu hiyo haina uwezo wa kifedha wa kujigharamia hususan pale inaposafiri kuelekea Unguja katika mechi zake.

Alisema kama ilivyo hivi sasa ligi inachezwa kwa vituo viwili, itafika wakati timu hiyo itashindwa kusafiri kutokana na kutokuwa na fedha za kujikimu kwa ajili ya kujiandaa na mechi.

Alisema analishukuru Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) kwa kugharamia nauli za wachezaji, lakini pia bado timu inahitaji fedha za kujikimu kama vile chakula, na sehemu ya uhakika ya kufikia inaposafiri hususan inapotua Unguja.

Alisema serikali kupitia wizara husika iangalie uwezekano wa kushirikiana na ZFF katika kutafuta wadhamini wa ligi hiyo ili kupunguza changamoto za kifedha.

# YANGA SC KUITAFUTIA PUMZI PYRAMIDS KWA PAN AFRICANS

**Na Mwandishi Wetu**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Yanga keshokutwa, Jumatano watashuka katika Uwanja wa Uhuru kuitafutia kasi Pyramids ya Misri kwa kuvaana na Klabu ya Pan Africans ikiwa ni baada ya leo kupasha misuli dhidi ya Friends Rangers.

Yanga itaikaribisha Pyramids Oktoba 27, mwaka huu katika Uwanja wa CCM Kirumba kwenye mechi ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kutolewa na Zesco ya Zambia kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika katika raundi ya kwanza.

Akizungumza na Nipashe kuelekea maandalizi ya kuivaa Pyramids, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema leo watakuwa na mechi ya ndani ambayo wataitumia kama kupasha mishuli kabla ya kuvaana na Pan Africans Jumatano katika Uwanja wa Uhuru.

"Baada ya mechi hiyo dhidi ya Pan Afrika tutajiandaa kwa safari ya kuelekea Mwanza Oktoba 20, mwaka huu kwani tunataka kufanya mazoezi ya nguvu na kuwawezesha wachezaji wetu kuuzoea vema Uwanja wa CCM Kirumba kabla ya kuikaribisha Pyramids," alisema Bumbuli.

Kuhusu leseni ya wachezaji wao wawili David Molinga 'Falcao' na Mustafa Seleman, Bumbuli alisema bado hawajapata taarifa rasmi ya kuwatumia kutoka Shirikisho la Soka Afrika (Caf) na kwamba wanaendelea kufuatilia ili kuweza kuwatumia katika mechi dhidi ya Pyramids.

"Bado Caf haijatoa leseni ya wachezaji hao ila tunaendelea kufuatilia na tunatumai mchakato huo unaweza kukamilika kabla ya kuvaana na Pyramids," alisema.

Yanga inaamini endapo Molinga atapata baraka za Caf kucheza mechi hiyo, atakuwa msaada mkubwa katika safu yao ya ushambuliaji ambayo imekuwa ikishindwa kutumia nafasi nyingi za kucheka na nyavu wanazotengeneza.

Aidha, ilieleza imeamua kuhamishia mechi hiyo katika Uwanja wa CCM Kirumba kutoka wa Taifa, kwa kile ilichokieleza ni kuwapa fursa pia mashabiki wao wali-



Mchezaji wa timu ya EFM (jezi nyekundu) katika harakati za kumiliki mpira dhidi ya beki wa Shekilango Boys, wakati wa mchezo wa Bonanza la EFM Muziki Mnene lililodhaminiwa na Benki ya NBC, ambao ulichezwa kwenye Uwanja wa Wachonga Vinyago, Mwenge jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Azam, African Lyon majaribuni

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuendelea kujiimarisha ili ifanye vizuri katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, kikosi cha Azam FC kinatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya African Lyon, itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru.

Azam FC itashuka dimbani leo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 5-0 walioupata katika mchezo mwingine wa kirafiki dhidi ya Green Warriors uliochezwa juzi usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

Ofisa Habari wa Azam FC, Jaffer Iddi, alisema jana kuwa mechi hiyo inachezwa kutokana na mapendekezo yaliyowasilishwa na benchi la ufundi la timu hiyo.

Iddi alisema wanaamini wachezaji watakaopata nafasi ya kucheza mechi hiyo, wataonyesha kiwango bora ambacho kinaweza kuwapa nafasi ya kuingia kwenye kikosi cha kwanza cha timu hiyo.

"Haya yote ni maandalizi yetu ya kuelekea mchezo wetu dhidi ya Simba, tunajua mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu tunacheza na moja ya timu ngumu, walimu wetu wanataka kuendelea kutumia vizuri mapumziko haya kujiimarisha zaidi," alisema Iddi.

Aliongeza kuwa mshambuliaji wao, Suleiman Ndikumana na beki na nahodha wa timu hiyo, Aggrey Morris, waliokuwa majeruhi, wamepona na wameanza kufanya mazoezi ya pamoja na wenzao.

Ndikumana alikuwa nje kwa muda mrefu na maumivu yake yalimfanya ashindwe kucheza mechi zote nne za Kombe la Shirikisho Afrika ambazo Azam ilicheza pamoja na michezo mitatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Oktoba 23, mwaka huu, Azam FC itavaana na Simba katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa kwenye Uwanja wa Taifa.

# Umaliziaji waitesa KMC Ligi Kuu Bara

**Na Mwandishi Wetu**

SUALA la umaliziaji limekuwa ni moja ya matatizo yanayokisumbua kikosi cha KMC FC ya jijini Dar es Salaam, ambacho kinashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa.

KMC FC ambayo imecheza mechi nne na ina pointi nne, iko katika nafasi ya 16 katika msimamo wa ligi hiyo yenye kushirikisha klabu 20 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa KMC, Mlage Kabange, aliliambia gazeti hili jana kuwa tayari wameanza kurekebisha tatizo hilo ili wafanye vema katika michezo inayofuata baada ya ligi hiyo kurejea upya.

**"Tumekuwa na tatizo la umaliziaji, washambuliaji wetu wanapoteza umakini wanapokuwa jirani na lango na wapinzani, wanatengeneza nafasi nyingi, lakini wanashindwa kumalizia, tumeliona na tunalirekebisha ili mechi zinazofuata lisijirudie tatizo hili," alisema Kabange.**

Kocha huyo wa zamani wa Kagera Sugar alisema ligi bado "mbichi", lakini kila timu inataka kuhakikisha inavuna pointi nyingi katika mzunguko wa kwanza ili kujiweka mahali salama kabla ya dakika za lala salama hazijafika. Mechi inayofuata ya timu hiyo ambayo itachezwa Oktoba 23, mwaka huu, itakuwa dhidi ya JKT Tanzania.

# Michezo

Jumatatu Oktoba 14, 2019

Nipashe




## Beckham ampongeza Ramos rekodi Hispania

HABARI UK 30



Kiungo wa Brazil, Arthur Melo akidhibitiwa na beki wa kushoto wa Nigeria, Jamilu Collins (kulia), wakati wa mechi ya kirafiki kati ya timu hizo iliyopigwa Singapore jana na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. Nigeria ilikuwa ya kwanza kupata bao dakika ya 35 kupitia kwa Joe Aribo kabla ya Casemiro kuisawazishia Brazil. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA KUITEKA KIGOMA LEO

## Aussems aichambua Mashujaa ilivyowatesa Kombe la FA, lakini asema hii ni timu...

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU ikiwa imepata mapokezi makubwa baada ya kuwasili mkoani Kigoma jana asubuhi, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wanatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya "wababe wao" Mashujaa FC inayotarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Mashabiki wa Simba kutoka sehemu mbalimbali mkoani humo, jana walijitokeza kuilaki timu hiyo kuanzia kwenye Uwanja wa Ndege, na kuisindikiza kwa magari, bajaj na pikipiki hali iliyofanya gari lililobeba wachezaji kupunguza mwendo.

Mara ya mwisho timu hizo zilikutana Desemba 25, mwaka jana katika mchezo wa mashindano ya Kombe la FA Tanzania na Mashujaa inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza ilifanikiwa kuiondoa Simba kwa penalti 3-2.

Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems amesema mechi hiyo ya leo inaendelea kuwaimarisha wachezaji wake ambao walikosa nafasi za kuonyesha viwango vyao kwenye michezo minne ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyotangulia.

Aussems alisema amefurahi juzi kupata mchezo mzuri dhidi ya Bandari FC ya Kenya, hivyo anaamini leo pia kikosi chake kinatarajia kukutana na ushindani kutoka kwa wenyeji wao, Mashujaa.

**"Najua haitakuwa mechi rahisi, tuna kumbuka walitu funga mwaka jana , lakini hii ni timu nyingine na huu ni msimu mwingine, matumaini yangu ni kuona mechi nzuri na yenye burudani," alisema Aussems.**

Kocha huyo aliongeza kuwa kila mechi husaidia kuimarisha sehemu fulani ya timu na ile inayoonekana kuwa na mapungufu, hufanyiwa kazi kwa ajili ya kufanya vema katika mchezo unaofuata.

Baada ya mechi hii, Simba itaendelea kubaki Kigoma na keshokutwa itawakaribisha Aigle Noir kutoka Burundi katika mchezo mwingine wa kirafiki utakaochezwa kwenye Uwanja huo huo kuanzia saa 10:00 jioni.

Ikirejea jijini, Simba itakutana na Azam FC katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Oktoba 23, mwaka huu, kwenye Uwanja

# Msuva, Kagere vitani Rwanda

**Na Somoe Ng'itu**

TIMU ya soka ya Taifa (Taifa Stars) inatarajiwa kuwakabili wenyeji Rwanda (Amavubi) katika mchezo wa kirafiki wa kimataifa utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Kigali (Nyamirambo) ulioko nchini humo.

Taifa Stars inatarajia kutumia mchezo huo kujiandaa na mechi yake ya marudiano ya kuwania tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) dhidi ya Sudan ugenini wakati Amavubi wenyewe wataikaribisha Ethiopia (Walias).

Katika mechi ya leo, Taifa Stars inamtegemea mshambuliaji wake anayecheza soka la kulipwa nchini Morocco, Simon Msuva, wakati Amavubi yenyewe itaongozwa na Meddie Kagere anayeichezea Simba ya jijini Dar es Salaam. Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Kocha Mkuu wa Taifa Stars Mrundi Etienne Ndayiragije, jana alisema wamejiandaa vizuri na wanatarajia mchezo huo utasaidia kuwaimarisha wachezaji wake ambao wengi hawana uzoefu na mechi za kimataifa.

Ndayiragije alisema anaamini mchezo wa leo utamsaidia kupata kikosi cha kwanza kitakachoivaa Sudan na amewataka wachezaji wake kutokuwa na hofu dhidi ya wenyeji hao ambao pia wanahitaji ushindi ili kuongeza morali.

Alisema hana majeruhi katika kikosi hicho, hivyo anaamini kila mchezaji atakayepata nafasi ataonyesha kiwango kizuri na kuisaidia timu kupata matokeo mazuri.

"Wachezaji wa Tanzania na Rwanda wanajuana, wanafahamiana, ni mchezo mgumu kwa kila upande, lakini utatuongezea maarifa kuelekea mechi inayokuja dhidi ya Sudan, kila mchezaji anatakiwa kuwa na nidhamu anapokuwa na mpira na kujua maeneo yake muhimu," alisema Ndayiragije.

Naye Kocha Mkuu wa Amavubi, Vincent Mashami, alisema mechi ya leo itakuwa na ushindani kutokana na kila nchi inahitaji kushinda ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye viwango vya Fifa, lakini kufahamiana kwa wachezaji kutaongeza changamoto. "Tumefanya maandalizi mazuri, tuna kikosi kizuri lakini chenye wachezaji wengi vijana, wamejiandaa kupambana kuhakikisha wanaendeleza matokeo mazuri, nimewaambia wasahau ushindi mkubwa tulioupata dhidi ya Shelisheli, huu ni mchezo mwingine, akili inatakiwa kuuangalia mchezo huu na si matokeo ya nyuma," Mashami alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >